JANUARI MMXXVI - TOLEO LA XLIX

# NGURUMO

*ya Mwandishi*




## MIEZI




## tumenguruma!

**HABARI KUU:**

•SOMO KANIPONZA, HADITHI YA MAANDISHI INAYOTAKA KUTEMBEA

**MAKALA:**

•SAFARI YA MIAKA MINNE YA NGURUMO YA MWANDISHI

## YALIYOMO

**TAHARIRI— Uk 02**
MIEZI 48 TUMENGURUMA

**MWANDISHI WETU— Uk 03**
DAVID SHALALI

**NEW IN TOWN: Uk 04**
AMEANDIKA AMOS BWIRE

**PITIO LA VITABU— Uk 05**
CHUNGU TAMU—4

**SAIKOLOJIA: Uk 06— 07**
UWE NA NGUVU YA KUPAMBANA NA MAUMIVU

**MAKALA: Uk 08 - 09**
MIAKA MINNE YA NGURUMO YA MWANDISHI

**KUTOKA KWA FANANI: Uk 10**
KAMBA ZA FRANK MASAI

**SAKO KWA BAKO – Uk 11**
MC PAULO

**RIWAYA: Uk 12—13**
MSALITI '10'

**RIWAYA: Uk 14—15**
Najutia Kuwa Na Wewe '11'

**YA KALE NI DHAHABU: Uk 16**
SAFARI 7 ZA SINDBAD BAHARIA

**HABARI MOTO: Uk 17**
SOMO KANIPONZA KUWA FILAM

**SHUBAKA LA VITABU: Uk 18**
TUNAMWANGAZIA TAHA HUSSEIN

**KITABU NILICHOSOMA: Uk 19**
MY LIFE MY PURPOSE

**MATANGAZO: Uk 22**

**MALENGA WA KILEO: Uk 21**
PONGEZI KWA NGURUMO na WAPE WATU WATU WAO

**HABARI PICHA: Uk 20**

**KUTOKA MAKTABA: Uk 23**
AGORO ANDURU

**ELIMU JAMII: Uk 24 & 25**
SAFARI YA MALEZI (8): MITINDO YA MALEZI

**HADITHI: Uk 26 - 27**
Happy New Year '13'

**HADITHI: Uk 28 - 29**
NGUVU YA KIAPO '08'

**KALAMU YANGU : Uk 30 - 31**

DIRA YA MOYO - LAURA PETTIE

## TAHARIRI:
## MIEZI 48 TUMENGURUMA

Nakusalimieni nyote popote mlipo,
Kwanza kabisa nikutakieni heri na baraka kwa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya. Najua sote tumesherehekea kwa amani na utulivu, tukiwa sambamba na familia zetu.

Ni jambo la kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kufika mwaka huu wa 2026. Si kwamba sisi ni bora sana, ila ni Mapenzi ya Mungu tu. Hivo tusijivune.

Lakini kwa namna ya pekee sisi nasi Ngurumo ya Mwandishi, Jarida maridhawa la kifasihi Tanzania linalokujia kwa nakala tepe tumefunga miaka minne na sasa tunauanza mwaka mpya wa tano wa kukufasihisha.

Haikuwa kazi ndogo kuandaa machapisho 48, lakini kwa msaada wa Mungu na mchango wako wewe msomaji tumefanikiwa. Na sasa tunapouanza mwaka huu wa 5 yaani machapisho ya 49-60 bado tunakutegemeeni ninyi yaani fanani na hadhira ili kufanikisha safari hii. Nikisema hivo namaanisha kwamba waandishi husimulia wanavyoandika na wasomaji husimulia wanavyosoma. Mambo ni bam bam.

Na kwenu ninyi wapenzi wasomaji, Ngurumo ya Mwandishi linakuandalieni zawadi nzuri sana kwenu nyote. Kaeni mkao wa kula.

Basi tuungane tena katika chapisho hili tukiangazia mwaka huu wa nne na majambo yake.

Wasalaam na muwe na Mwaka Mpya mwema!

C.E.O - Richard Mwambe

*Richard Mwambe*

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

# MWANDISHI WETU:
## DAVID SHALALI

**KATIKA safu yetu ya Mwandishi Wetu, leo tunaye 'nguli - kisiki' David Shalali. Huyu ni mwandishi anayetamba na riwaya yake ya Salome wa Sadaka pamoja na nyinginezo. Huyu ni 'Kumi Bora' bora kabisa wa Tuzo ya Nyerere ya Uandishi Bunifu. Yupo hapa kurasani, karibu umsome na umjue...**



Mimi ni mwandishi wa vitabu kutoka Tanzania, ninaishi Jijini Dar es Salaam. Nimejipambanua kama mwandishi mahiri wa riwaya na tamthilia, huku nikijaribu pia kalamu yangu katika mashairi kwa uchache. Jina langu ni David Shalali.
Kupitia maandishi yangu, ninajaribu kuonyesha dhamira ya dhati ya kuitumia fasihi kama kioo cha jamii, chombo cha burudani, na darasa la elimu kwa wasomaji wake.

Safari yangu ya uandishi ilianza tangu utotoni nilipokuwa shule ya msingi. Tangu wakati huo, nilionesha kipaji cha pekee cha kupenda kwa kusimulia na kuandika hadithi zilizoakisi maisha halisi ya watu walionizunguka. Kichocheo kikubwa cha mimi kuwa mwandishi kilitokana na hamu ya kueleza uhalisia wa maisha ya jamii ya Kitanzania, hasa changamoto zinazowakabili vijana na makundi mbalimbali ya kijamii.
Hata hivyo, safari haikuwa rahisi. Miongoni mwa changamoto kubwa nilizokutana nazo mwanzoni ni gharama za uchapishaji, hasa nikiwa kama mwandishi na mchapishaji binafsi. Licha ya vikwazo hivyo, sikukata tamaa. Hatua muhimu katika kujijenga kwangu ilikuwa ni kujiunga na Umoja wa Waandishi wa Riwaya wenye Dira maarufu kama UWARIDI, Umoja huu ndio ulionipa mwanga, uzoefu na hamasa vilivyonijenga hadi kufanikisha kutoa kitabu changu cha kwanza nilichokipa jina Salome wa Sadaka.

Pia nimeandika vitabu kadhaa ambavyo ninaamini vitaaacha alama katika tasnia ya fasihi. Miongoni mwa kazi zangu muhimu ni, Salome wa Sadaka (Riwaya ), Beti ya Mauti (Tamthilia iliyotajwa kwenye tuzo ya Taifa ya Mwalimu nyerere), Siri ya Mke Wangu (Itazinduliwa mwaka huu)
Hapa naweza nikasema kitabu kilichonipatia mumaarufu mkubwa zaidi ni Salome wa Sadaka pamoja na Hadithi ya Siri ya Mke Wangu ambayo ilipata mvuto mkubwa ilipokuwa ikirushwa mtandaoni.

Huwa ninaandika kwa lugha rahisi na inayoeleweka kwa wasomaji wa rika mbalimbali. Mtindo wangu umejikita zaidi katika uhalisia, nikitumia matukio yanayofanana na maisha halisi ya jamii ya Kitanzania. Kazi zangu mara nyingi huwa ni za kufikirisha, kuburudisha na kuelimisha kwa pamoja, jambo linalonifanya niwe mwandishi ninayekubalika na makundi tofauti ya wasomaji.
Kwa mchango wangu katika fasihi, nimepata kutambuliwa kitaifa kupitia Tuzo ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu ambayo hutolewa na serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania. Mwaka 2023, nlitajwa mshindi wa sita katika kipengele cha riwaya, na mwaka 2025 nikawa mshindi wa tisa katika kipengele cha tamthilia. Umaarufu wa vitabu vyangu unaendelea kukua, hasa kupitia mauzo na maoni ninayoyapata kutoka kwa wasomaji.

Wasomaji wengi wamekuwa wakitoa maoni chanya juu ya kazi zangu. Moja ya maombi yanayojirudia ni kutolewa kwa mwendelezo wa riwaya ya Salome wa Sadaka kutokana na jinsi ilivyowagusa na kuwabamba. Wengine wamefikia kunifananisha uandishi wangu na mwandishi nguli wa Tanzania, Mzee Faki A. Faki, wakitaja uwezo wake wa kusimulia hadithi zenye uzito wa kijamii. Sifa kubwa ni uhalisia na lugha rahisi ninayotumia, taharuki ninazozijenga japo huku changamoto kubwa ni namna ya kuwafikia wasomaji wengi Zaidi.

Kwa ujumla, Mimi ni mwandishi ambaye ninatoa mchango mkubwa katika kukuza fasihi ya Kiswahili, hasa kupitia riwaya na tamthilia zinazogusa maisha ya kila siku ya jamii. Ninafaa kusomwa na kuigwa kwa sababu ya uthubutu wangu wa kuandika uhalisia bila kuficha, pamoja na nidhamu na uvumilivu nilioonyesha katika safari yangu.

Kwa waandishi chipukizi, funzo kubwa kutoka kwangu ni kwamba kipaji, uvumilivu na kujifunza kutoka kwa wengine ni nguzo muhimu za mafanikio.

## Ameandika Amosi Bwire 'Baba BM'

Wiki mbili zilizopita, wakati nachukua mzigo wangu wa vitabu kwenye dawati lake, rafiki (mlinzi) wa mapokezi alinitazama, akaniuliza; "Kwa nini unapenda sana vitabu?" Nikamwambia, "Huwa naishi maisha mazuri sana ndani ya vitabu, kuliko ninayoishi nje ya vitabu."
Hakunielewa. Sikumwelewesha. Tukaishia kucheka, nikaenda kuendelea kuwajibika.

Ifuatayo ni orodha ya baadhi ya vitabu nilivyonunua mwaka 2025. Nimegusagusa kadhaa, ila nimemaliza tisa tu!
Kipi hapo umeshakisoma na ungependa mwingine naye akifaidi?

1. The Book Thief (Markus Zusak)
2. Uswahilini (Ally Mchanyato)
3. The Seven Deaths of Evelyn Hardcastle (Stuart Turton)
4. The Wrong Side of Goodbye (Michael Connelly)
5. The Last Place You Look (Louisa Scarr)
6. Year One (Nora Roberts)
7. Mwandae Mtoto Wa Kiume Kuwa Mwanaume (Hanifa Kafashe)
8. Things We Never Got Over (Lucy Score)
9. Flawed (Cecelia Ahern)
10. The Perfect Life (Jo Spain)
11. Ujanajike (Dotto Rangimoto)
12. Sleep No More (P.D James)
13. The Messiah Secret (James Becker)
14. Gone For Good (Harlan Coben)
15. Sundays At Tiffany's (James Patterson)
16. The Quickie (James Patterson)
17. The Angel's Game (Carlos Zafòn)
18. Ndoa Ya Kikristo (Henry Mchamungu)
19. Gereza La Kifo (Hamisi Kibari)
20. The Woman Who Stole My Life (Marian Keyes)
21. Man's Search For Meaning (Viktor Frankl)
22. My Sister, The Serial Killer (Oyinkan Braithwaite)
23. Dying For Christmas (Tammy Cohen)
24. The Perfect Wife (J.P Delaney)
25. Ask For It (Sylvia Day)
26. Marriage On Trial (Stanton & Maier)
27. Harufu Ya Kifo (Kamanda Amata Ric)
28. I Let You Go (Clare Mackintosh)
29. The Perfumed Garden (Muhammad al-Nefzawi)
30. The Book Of Souls (James Oswald)
31. No Angel (Penny Vincenzi )
32. Their Little Secret (Mark Billingham)
33. This Charming Man (Marian Keyes)
34. The End Of Men (Christina Sweeney)
35. Unwavering (Nellie Borrero)
36. Joe Country (Mick Herron)
37. Come The Spring (Julie Garwood)
38. Dust (Patricia Cornwell)
39. Long Time No See (Susan Isaacs)
40. Never Never (James Patterson)
41. Tomorrow, And Tomorrow, And Tomorrow (Gabrielle Zevin)
42. Shattered (James Patterson)
43. Mr Nobody (Catherine Steadman)
44. No Turning Back (Susan Lewis)
45. The Missing Wife (Sheila O'Flanagan)
46. Msaliti (Kamanda Amata)
47. Passion For The Game (Sylvia Day)
48. Countdown (Iris Johansen)
49. Signs Of Life (Dr David Jeremiah)
50. Fanani (Zainab Baharoon)
51. One Hit Wonder (Lisa Jewell)
52. The Book Of Two Ways (Jodi Picoult)
53. The Lying Game (Ruth Ware)
54. Meno Ya Mbwa (Kalmas Konzo)
55. The Fault In Our Stars (John Green)
56. Just One Of Those Flings (Candice Hern)
57. A Return To Love (Marianne Williamson)
58. Murder On The Down Low (Pamela Young)
59. Shame (Jasvinder Sanghera)
60. The 6:20 Man (David Baldacci)
61. Blow Fly (Patricia Cornwell)
62. Obsessed (James Patterson)
63. In One Person (John Irving)
64. Bad Love (Jonathan Kellerman)
65. The Moscow Rules (Antonio Mendez)
66. Can't Get Enough (Connie Briscoe)
67. Mercy (David Baldacci)
68. The Legend Of Sheba (Tosca Lee)
69. Good In Bed (Jennifer Weiner)
70. Pieces Of Her (Karin Slaughter)
71. I Will Find You (Harlan Coben)
72. Hard Girls (Martina Cole)
73. Mapenzi Yamelogwa (Hussein Wamaywa)
74. The Seven Husbands of Evelyn Hugo (Taylor Jenkins)
75. Muuaji Wa Mwaka Mpya (Hussein Tuwa)
76. Nimesamehe, Nimeachilia, Nimejisamehe (Eva Mrema)
77. Beware A Scots Revenge (Sabrina Jeffries)
78. Therapy (Jonathan Kellerman)
79. Rage Of Angels (Sidney Sheldon)
80. The Sky Is Falling (Sidney Sheldon)
81. Kamusi Kuu Ya Kiswahili (BAKITA)
82. Kosa Langu (Vennita Mwita)
83. Bad Girls (Rebecca Chance)
84. A Glasgow Kiss (Sophie Gravia)
85. The Birthday Present (Barbara Vine)
86. A Million Little Pieces (James Frey)
87. Cheater (Karen Rose)
88. The Tea Planter's Wife (Dinah Jefferies)
89. The Castaways (Lucy Clarke)
90. Sijaorodhesha nakala laini.

# Diwani - CHUNGU TAMU (4)



**DIWANI YA CHUNGU TAMU**

**MWANDISHI: THEOBALD MVUNGI**

**WACHAPISHAJI: TPH**

**MWAKA: 1985**

**Inatoka toleo lililopita…**

Shairi la *"Chini ya Mti Mkavu"* mwandishi analaani uongozi unaoendeleza dhuluma katika jamii. Anakemea juu ya uongozi mbaya usiojali maslahi ya wengi, uongozi usiopiga vita umaskini hapa nchini, n.k.

Katika shairi la *"Wanajua Kuvumilia"*, mwandishi analaani ahadi za uongo zinazotolewa na viongozi wetu. Ameonesha kuwa viongozi wetu hawasemi ukweli bali uongo ndio umetawala midomo yao. Katika shairi hili mwandishi analaani vibaya viongozi ambao hawafiki vijijini kwa wananchi waliowachagua ili kujionea hali halisi ya maisha wanayoshi.Mwandishi anasema:-

*"Afadhali kuimba ukweli,*

*Wimbo mchomo mkali,*

*Wimbo, unalilia hali,*

*Ya vijiji vilivyo mbali,*

*Kwa wale wasio kauli."*

Katika shairi la *"Udongoni"* mwandishi anawakumbusha viongozi wajibu wao katika jamii. Mwandishi anasema:-

*"Lanikumbusha wajibu,*

*Kujenga si kuharibu,*

*Naahidi kujaribu,*

*Kulinda tulichojenga."*

Mwandishi anaona kuwa Uongozi bora ni msingi mkubwa katika ujenzi wa jamii mpya hivyo anaiasa jamii kupiga vita Uongozi mbaya ili kujenga jamii endelevu hapa nchini.

4. **KUWEPO NA DEMOKRASIA YA KWELI**

Demokrasia ni mfumo wa kuendesha serikali iliyochaguliwa na watu kwa manufaa ya watu wenyewe. Demokrasia inahitajika sehemu yoyote ile ili kuwaruhusu wananchi kutoa maoni yao kwa uhuru bila wasi wasi au kikwazo chochote. Katika shairi la *"Mjanja yu Mashakani"* mwandishi anasema;

*Kumezuka mkatao, miaka ya themanini,*


*Watu wafanya jutio, hawasemi chinichini,*

*Hawasemi tena ndio, haitoki midomoni,*

*Wamevumilia sana, mwisho wa uvumilivu.*

Mwandishi anajadili kuhusu mfumo wa demokrasia ambao umejitokeza miaka ya 1980 kote ulimwenguni. Mfumo huu ni ule wa kupinga sera ya chama kimoja na kuingia katika mfumo wa vyama vingi (mageuzi). Katika shairi hili mwandishi anaonesha kuwa mfumo wa vyama vingi umewaamsha wananchi wengi kutoka usingizini na kuanza kutetea haki zao. Hata hivyo, mwandishi anaonesha kuwa wale viongozi waliojilimbikizia madaraka na vyeo mbali mbali wamehofia sana mfumo huu na hivyo hufanya kila mbinu ili kuudidimiza. Viongozi wanaong'ang'ania madaraka ndio wanaohofia mfumo huu.

Shairi la *"Kademokrasi Kametoweka"* linapinga uongozi mbaya barani Afrika. Mwandishi ameonesha kuwa demokrasia inapopokonywa na viongozi wachache, udikteta huota mizizi na kuung'oa huchukua muda




mrefu. Hali hii inasababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe katika baadhi ya nchi barani Afrika. Mfano wa nchi hizo ni Jamuhuri ya Watu wa Kongo, Uganda, Burundi, Sierra Leone, n.k. Utawala wa nguvu hurudisha nyuma maendeleo ya bara la Afrika na nchi nyingine za ulimwengu wa tatu ambako hakuna demokrasia ya kweli. Mwandishi anasema:-

*"Barani mabavu yatumika,*

*Dikteta asijeanguka,*

*Na majungu pia ayapika,*

*Udikteta pasi shufaka,*

*Nasimulia ya Afrika*

**Itaendelea toleo lijalo...**

# -SAIKOLOJIA-

## UWE NA NGUVU YA KUPAMBANA NA MAUMIVU.



Na. Madam Neema Mgao

**UWE NA NGUVU YA KUPAMBANA NA MAUMIVU**

Ni mwisho wa mwaka tayari, 2025 tumeimaliza. *Happy New Year* mpendwa rafiki yangu. Tumeivuka salama 2025. Ile mipangilio mizuri tuhamie nayo 2026, na yale yaliyotuumiza tuyaache kulekule nyuma. Mwaka mpya na mambo yawe mapya.

Mpendwa wangu, Mungu hakukosea kukuumba, wala hakukosea kuruhusu uzaliwe ukitokea tumboni kwa mama yule, na pia alikua na makusudi yake aliporuhusu utokee kiunoni kwa baba yule. Kisitokee chochote katika kukufanya ukate tamaa ya kuishi duniani. Chochote ulichopitia mwaka jana, kiache kulekule. Usibebe maumivu yake, bali beba yale mazuri yote anza nayo na uyaendeleze katika safari ya maisha kwenye mwaka 2026

HAPPY NEW YEAR RAFIKI YANGU!

Katika makala hii ya kufungia na kufungulia mwaka, nataka tuzungumze kisaikolojia kuhusiana na NGUVU YA KUPAMBANA NA MAUMIVU.

**MAUMIVU NI NINI?**

Maumivu ni hali ya moyo au nafsi kupata hisia ziumizazo. Ni hali itokeayo ikiambatana na hisia za kuumia au kuumiza.

**AINA ZA WATU NA MAPOKEO YAO YA MAUMIVU**

Mungu aliumba watu tofauti tofauti. Tuangalie aina tatu za watu katika mapokeo ya hasira.

**A]. Wanaoonyesha maumivu wakiumia.**

Hii ni aina ya watu ambao wakiumizwa huonyesha namna wanavyoumia, hili ni kundi la watu ambalo unapomuumiza hawezi kuweka hizo hisia za maumivu moyoni, hawa ni watu ambao wanaweza kukwambia hapo hapo kuwa umewaumiza. Hawa ni watu ambao hawawezi kuweka hasira wala kisasi moyoni, ni nadra sana kuweka kisasi kwani wakiumizwa hawakubali kukaa na maumivu.

**B]. Wanaoficha maumivu wakiumia.**

Hii ni aina ya watu ambao ni ngumu kuishi nao, hawa huwezi elewa kama wamekasirika wala huwezi elewa kama wamefurahi. Wapo watu walioumbwa kwamba wakipitia nyakati za kuumiza wao wanakua imara sana, hautomuona akiteteleka. Tofauti ya watu hawa ni ule uwezo wa kuhimili hisia ziumizazo, lakini si kweli kwamba eti hawaumii. Wanaumia ila wanaficha hisia zao, wapo radhi kwenda kulilia chooni, hawakubali kuonekana dhaifu, hawakubali kuonekana wameumia. Hawa huweza kuhimili maumivu na wanaweza kutunza visasi.

**C]. Wapuuziaji au wasioeleweka.**

Hawa ni watu ambao wao wakichukia hawaonyeshi na wala wakifurahi pia huwezi kuwajua. Hawa huitwa wapuuziaji au waweza watafsiri kama watu wasioeleweka.

Makundi yote hayo matatu ni vyema kujielewa kuwa upo kundi gani kisha uwe na nguvu ya kupambana na maumivu. Unaweza kuonekana kami ni imara kwa nje, au kwamba wewe huwa huumii, kumbe ndio wale ambao unaweza kuihifadhi hasira ya kuudhiwa hata kwa miaka mitano, ukiulizwa unasema *"haiishi mpaka iishe"*.

**Unawezaje kutengeneza nguvu za kuhimili maumivu?**

Zipo njia nyingi ambazo unaweza kuzitumia ili kuhimili hisia za maumivu.

**- SAIKOLOJIA -**

# UWE NA NGUVU YA KUPAMBANA NA MAUMIVU.

**1. Pokea kuumia.**

Kwakua wewe ni binadamu nyakati za maumivu hazina budi kukuandama. Pokea kuumia. Lolote linalotokea na likakuumiza pokea kuumia ili usiteseke.

**2. Ruhusu kuumia.**

Ruhusu hiyo hali ya maumivu. Ruhusu kuumia. Ili moyo na akili yako visiumie sana basi ni muhimu kuruhusu kuumia. Zingatia kuwa wewe ni binadamu, maumivu na furaha ni lazima kupitia hali hizo.

**3. Umia**

Umia, pokea kuumia, ruhusu kuumia, umia. Tena usijizuie kuumia, umia haswa huku ukijitamkia uponyaji wa hisia hizo za maumivu.

**4. Tibu maumivu**

Hii ni hatua muhimu sana katika maisha ya mwanadamu. Usikubali maumivu yakadumu moyoni mwako. Tafuta tiba ya maumivu hayo. Tibu kwa kuzungumza na watu, Toa hisia zako za maumivu, Sikiliza muziki uupendao ili kuifariji akili yako, au fanya kile upendacho ili kujitibia maumivu yaliyokusonga.

**Jisahaulishe maumivu**

Inaweza kutafsirika kama kupuuzia, ila ni tofauti kidogo. Kupuuzia ni kufanya kama hakijatokea kitu, ila hapa tunazungumzia kujisahaulisha. Kwamba moyo unakiri kuwa kitu kimewahi kukuumiza ila sasa ni muhimu kuacha yapite, unafanya kama haijawahi kukutokea.

Kusanya nguvu ya asili ili kuweza kuhimili nyakati za maumivu. Hauwezi kupata amani nyakati zote, nyakati chungu na zenye maumivu hazina budi kutokea. Zikitokea ni vyema kuzikabili, kuzidogosha na kuziondoa kwa nguvu ya asili ili amani na raha viweze kutuandama kwa mwaka 2026.

Happy new year mpendwa rafiki yangu. 2026 ikajae Amani na raha tele. Mungu atubariki sote.

**Kwa unaehitaji ushauri usisite kuwasiliana nami kupitia +255763013206.**

**MADAM NEEMA MGAO.**
**DODOMA.**
**TANZANIA.**

SOMA VITABU

- Kwa afya ya ubongo wako
- Kwa kujiongezea maarifa
- Kwa burudani

USISITE

- Kumsimulia mwingine hadithi uliyosoma
- Kumfundisha mwingine yale uliyojifunza
- Kumshauri mwingine kitabu cha kusoma

NI VIZURI

- Kutembelea maktaba
- Maduka ya vitabu
- Kupiga stori na waandishi

official KITABU Market
www.kitabumarket.co.tz
scan here and enjoy

**Je; unataka kuhaririwa, kuandikiwa (ghost writing), kuhakikiwa au kuchapiwa hadithi au kitabu chako?**

**Wasiliana nasi kwa**
**Whatsapp: 0766974865**
**Call: 0672160016**

**Gharama zetu ni nafuu mno… mpaka mwenyewe utashangaa…!**

# MIAKA MINNE YA NGURUMO YA MWANDISHI

## Jarida Maridhawa la Ufasihishaji Hamasishi Tanzania

KAMA ni mtoto basi apaswa sasa kuingia Chekechea. Mtoto aliyezaliwa katika hali isiyotegemewa sasa amekuwa gumzo ndani na nje ya nchi kwa wote wanaopenda fasihi ya Kiswahili.

Ameshakufikia zaidi ya mara arobaini na nane (48) katika maisha yako, akikusimulia hadithi, akikupa elimu mbalimbali za kijamii na burudani nyingine za ushairi na kukuonesha picha kemkem za kifasihi. Mtoto huyu ni mwanafasihi anayekuhamasisha wewe kuwa mpenzi wa fasihi kwa ujumla. Mwangwi wa uhamasishaji wake umesikika kwa miezi arobaini na tisa sasa kupitia mitandao ya kijamii, Tanzania mpaka Kenya, Burundi na Rwanda mpaka Congo, achilia mbali Afrika Kusini mpaka Misri, na Ujerumani, Uingereza, Italia, Uhispania na Marekani. Kote huko mwangwi wake unasikika, sifa zake zinasifika. Huyu si mwingine ni NGURUMO YA MWANDISHI.

Hili ni jarida maridhawa la ufasihishaji hamasishi. Linahamasisha jamii kuipenda fasihi, linatumia fasihi kuielimisha jamii na kuiburudisha, achilia mbali kuikosoa na kuinyoosha. Linawatangaza wanafasihi na kuwafikisha kwa wasomaji, wao na kazi zao. Ngurumo ya Mwandishi ni zao jingine kutoka Jamvi la Simulizi.

## Wazo lilitoka wapi?

Wazo la kuwa na jarida hili maridhawa lilianzia pale Msasani Beach Oktoba '21. Niliketi nikiwa na gazeti mkononi mwangu. Sikuwa peke yangu, nilikuwa na rafiki yangu kipenzi Rehema Stanley Kamana (Rey Stanley) *'Aendelee kupumzika kwa amani'*. Aliniuliza, "hivi hatuwezi kuwa na kitu kama jarida hivi ambalo litakuwa na simulizi za waandishi wachanga kwa wakongwe na mambo kadhaa ya elimu?" hili lilikuwa swali tunduizi. Ambalo mara moja akili yangu ilianza kufikiri na kuzunguka huku na huko.

"Ndiyo inawezekana, lakini unafikri itakuwa njia nzuri kuwafikia wafuasi wetu?" nilimuuliza. Naye akajibu "Tujaribu tuone, tunaweza kufungua milango mipya, maana sisi tutaandaa na wao watatawanya," maneno haya yalinipa nguvu ya ajabu. Juma lililofuata tayari nilikuwa nimefikiri kitu cha kufanya. Lakini tatizo likawa, jarida hilo liitweje?

Ngurumo ya Mwandishi ni jina moja kati ya mengi ambayo Hayati Rey Stanley alilichagua. Basi kazi ikaanzia hapo. Nilikuwa naandika na kukusanya maandiko ghafi kutoka kwa waandishi wengine na mitandao kisha yeye alikuwa mkaguzi wa mwisho kabla hatujalitoa kwa wasomaji.

Mpaka anafariki, ndiye alikuwa jicho la mwisho la kutazama na kusema sasa tuwape wasomaji.

### Ugumu wa Safari ya Ngurumo ya Mwandishi

Safari ya Ngurumo ya Mwandishi imekuwa ngumu sana, ngumu kuliko unavyofikiri. Lakini hata nilipobaki peke yangu sikukata tamaa. Uandaaji wa jarida hili unahitaji watu. Watu ambao watakupa makala hii, watakupa hadithi ile, wataandika hiki na watakubali kuandikwa wao. Lakini wakati mwingine ahadi zao za kukupa hayo maandishi hazitimiliki mpaka siku ya kutoa jarida. Hivyo inakubidi sasa mwandaaji kuzurula.

Utengenezaji wa *graphics* nao ni sehemu nyingine ya changamoto, wenye *software* wanataka pesa kubwa, wenye ujuzi wanaringa nao. Basi, lakini tunamshukuru Mungu kwa kile alichotupa tunakitumia. Wengi wamekuwa wakiuliza "unatumia softwea gani", jamani hii ni Microsoft Publisher ya mwaka 2010.

Ukiachana na yote hayo, muda nao umekuwa tatizo jingine, wakati unatakiwa kuandaa jarida bado una kazi zingine za kufanya. Jarida hili haliandaliwi kwa siku moja au masaa kadhaa bali kwa mwezi mzima au hata zaidi. Inakubidi kila siku kushika kompyuta na kufanya kitu fulani. Lakini amini usimini sasa tupo toleo la arobaini na tisa.

Wapo ambao waliazimia kufanya kitu kama hiki, palikuwa na majarida mazuri kabisa kama Tulizo, Kalamu Tulivu na jingine nimelisahau jina lakini hayakuweza kuendelea nadhani sababu ni hizi hizi changamoto.
Sisi Ngurumo, tumevumilia na kupambana mno. Wakati mwingine tumekata tamaa lakini washabiki wametufanya tusimame na kuendelea mbele.

### Falsafa ya Ngurumo ya Mwandishi

Jarida la Ngurumo limejikita katika falsafa kuu ya '*Mwandishi ni dha-*

*miri ya jamii'*. Hii inamaanisha

a. Kuandika ni jukumu la kimaadili

b. Ukimya wa mwandishi mbele ya uovu ni aina ya usaliti

c. Fasihi ni silaha ya kupinga upotoshaji na dhuluma.

Katika miaka hii minne sisi Ngurumo ya Mwandishi kwa kukutana na kuzungumza na waandishi tumejifunza na tumeamini kuwa uandishi huanza ndani ya mwandishi mwenyewe. Kabla ya kuikosoa jamii, mwandishi huitazama nafsi yake; kabla ya kuhubiri haki, hujifunza unyenyekevu; kabla ya kutoa sauti, husikiliza. Hivyo uandishi ni safari ya kiroho, kimaadili na kiakili.

Hatuhubiri ukamilifu wa lugha bila dhamira. Tunathamini uzuri wa lugha, lakini zaidi tunathamini uzito wa ujumbe. Lugha iwe safi, lakini ukweli uwe hai, hata pale unapouma.

Ngurumo ya Mwandishi inalenga kujenga urithi wa fikra. Na hii ni kwa sababu tunatambua kwamba

*'Neno lisilosemwa linaweza kuwa kosa, na neno linalosemwa kwa ujasiri linaweza kuwa mwanzo wa mabadiliko'.*

Kupitia jarida hili, wapo watu wamebadili fikra zao, wamebadili namna ya kuishi, na wamebadili mtazamo wao katika suala zima la 'fasihi ni kazi'. Kwa sababu jarida hili husomwa na watu wote wa rika lote.

## Faida

Kiukweli, Ngurumo ya Mwandishi hatupati faida yoyote kifedha. Imekuwa kama kazi ya kujitolea kwa mapenzi yetu ya fasihi. Nasi tunafurahi kufanya hivyo maana huu ni wito. Hata wote wanaochangia makala, hadithi, elimu hakuna anayelipwa kila mmoja analeta kazi kwa upendo wake. Cha msingi tunafahamiana na watu, tunafika kwenye majukwaa makubwa ya kimataifa. Na mpango wetu kwa sasa ni kulifikisha Ngurumo mbali zaidi.

## Shukrani

Haitapendeza kama makala hii itatamatika pasi na kuwasukuru watozi wote tunaoshirikiana nao. Shukrani zetu kwa majina ziende kwa Madam Neema Mgao, huyu amekuwa mstari wa mbele kutoa elimu ya Saikolojia kwa wasomaji. Bi. Eva Mrema, Asha Siraji, Twahir Yusuph, Makoleko Kalibonge na waandishi wengine waliotupatia hadithi za kuweka humu bure. Tunamshukuru Kelvin John Kyara kwa kutuletea elimu ya malezi kwa wazazi. Tunawashukuru sana Anna Mbise Mobile Library kwa kutupatia chambuzi za vitabu. Zaidi tunakushukuruni ninyi wasomaji wote maana mnalipeperusha mbali sana jarida hili.

Basi nikuombeni nyote, tuendelee kuwa pamoja na kulisambaza jarida hili nje ya mipaka ya Tanzania.

## Tuzo

Mwaka 2025 Mwasisi wa Ngurumo ya Mwandishi, Bw. Richard Mwambe alipokea Tuzo ya Heshima kwa kupitia jarida hili. Tuzo hiyo ilimtambua kama mwanaharakati wa fasihi ya Kiswahili tanzania aliye hai. Tuzo ilitolewa na Tanzania Fasihi Fund. Tunaamini kabisa kuwa ipo siku hata tuzo za Kimataifa zitafika.

*Happy New Year* kwenu nyote!




Bw. Richard Mwambe, mwasisi wa Ngurumo ya Mwandishi na C.E.O wa Jukwaa la Jamvi La Simulizi. Mmoja wa waandishi mahiri wa riwaya Tanzania.

## *Porojo na Kamba* Za Frank Masai : Urafiki wangu na Amita Batchan

Nakumbuka Mwaka 1974 Nikiwa Kwenye Kampuni Fulani Hivi ya Kutengeneza Baruti Iliyokwepo Kule Bombay India, Wafanyakazi Walianzisha Migomo Wakidai Nyongeza za Mishahara na Marupurupu Mengine. Suala Lile Lilikuwa Kubwa Sana Pale Bombay Kiasi cha Kutishia Amani Kwani Wafanyakazi Walianza Kutengeneza Fataki Chini ya Kiwango.

Ndipo Boss Mkuu Pamoja na Mabosi Wengine Kama Mimi na Mwenzangu Amitha Bachan, Tuliitisha Kikao cha Jinsi ya Kufanya Hilo Viguvugu Litokomee kwa Muda Wakati Kampuni Inajipanga Kurekebisha Malalamiko ya Wafanyakazi. Ni Ukweli Usiopingika, Kampuni Ilikuwa Inapitia Hali Mbaya ya Kiuchumi Kama Walivyo Wafanyakazi.

Kulikuwa na Njia Kadhaa za Kurekebisha Suala Hilo, Ikiwemo Kupunguza Wafanyakazi na Watakaopungua Mishahara Yao Ikimbizwe kwa Watakao Baki. Hii Ilikuwa Option Kubwa na ya Kwanza. Lakini Option ya Pili, Hii Ilikuwa ya Boss Wetu Ambaye Hata Hivyo Hakupendwa na Wafanyakazi Wengi na Hata Baadhi ya Mabosi. Wengi Wetu Tulimchekea Usoni Sababu Ndiye Boss Wetu na Kama Ujuavyo Boss Hanuniwi. Lakini Deep Down, Hatukumpenda. Hata Ingia Yake Kwenye Kampuni na Kuwa Boss, Haikuwa Inafahamika.

Sasa Hii Option ya Pili, Boss Aliitoa Akijua Wazi Hapendwi Hivyo Alitaka Kutumia Chuki Hizo Kubadilisha Upepo Ambao Ulikuwa Unasambaza Moto kwa Kasi ya Ajabu. Option Hii Haikuwa na Lengo la Kupunguza Wafanyakazi Wala Kuongeza Mishahara. Hii Lengo Lake Lilikuwa ni Kuwafanya Wafanyakazi Wawe Bize Kujadili Ishu Zingine Wakati Huo Wakifanya Kazi ya Kampuni kwa Usahihi.

Guess What?

Boss Alitoa Option Yake, Akasema Huu Mpango Wangu Nauita Terminator Ya Quartier. Akitumia Slang ya Kikongo kwa Maana ya Kuwa Mpango Wake Unaweza Kusimamisha Kila Kitu; Terminator Ya Quartier. Kisha Akasema Nakutuma Wewe Don Franco Masai a.k.a Kata Ndombe uende ukatumikie mpango huu sambamba na Amitha Bachani.

Kabla Hajaendelea Nikamuuliza Maana ya Kata Ndombe. Akacheka Sana. Kisha Akaniambia Amekaa Sana Pale DRC, Hivyo Anaimanya Lingala Kiasi Chake. Akaniambia Kuwa, Kata Ndombe Maana Yake ni Kijana Mwenye Sifa ya Urefu, Weusi na Utanashati; Kata Ndombe.

Kwa Mwili Wangu We Utaniona Sina Urefu Wowote. Ila Kwa Boss Wangu na Wafanyakazi Wengine, Nilikuwa Mrefu Sana, The Giant. Na Huu Weusi Plus Zile Suti Zangu, Oya Kata Ndombe Huyu Hapa.

Ule Mpango Ukawekwa Mezani, Kata Ndombe Nikaambiwa Mimi Nikaanzishe Mada ya Kuwatetea Wafanyakazi. Akanipa na Jopo Litakalo Nisaidia. Halafu Baada ya Siku Moja Amitha Bachan Aje Kuipinga Ile Mada Akiwa na Jopo Lake Pia. Tulipomuuliza Kwa Nini Iwe Hivyo, Akajibu Kafanyeni Nilichowatuma, Mtayaona Matokeo.

Basi Kata Ndombe na Jopo Langu Tukatoka na Kesho Yake Tukaanza Kutetea Wafanyakazi kwa Pointi Murua Kabisa. Pointi za Kisomi, Pointi Zenye Poor Hair Dressing (PHD). Soon Tukavutia Wafanyakazi Wengi Mno.

Kesho Yake Akaja Mzee wa *Roterote Asnasiko, Aste Astee Kooona*. Uncle Amitha Bachan. Yeye Akadai Mimi Nawapoteza Wafanyakazi. Kwanza Mimi ni Muafrika, iweje Leo Nisimame Sambamba na Wahindi? Hata Cheo Chenyewe Nimepewapewa Tu! Je, Ni Kweli Mimi na Maumivu Kama ya Wenye Nchi Yao?

Bachani Akatoa Pointi Nyingi Sana Zilizokwenda Sambamba na Ubaguzi Pamoja na Kujigawa. Soon, Yale Malalamiko ya Wafanyakazi Yakaanza Kupotea, Na Wakajikita Kwenye Kujadili Rangi Yangu, Imani Yangu na Hata Maisha Yangu. Haikuwa Kwangu Peke Yangu, Hata Wale Wahindi Weusi Wlijadiliwa Vivyo Hivyo. Wahindu, Mabudha, Monki na Waterugu Wote Wakaanza Kutengana.

# SAKO KWA BAKO:

## PAUL KUSEKWA 'MC PAUL': VITABU NA MIC'

**Katika Sako kwa Bako, leo tunaye MC machachari kabisa kutoka huko Kanda ya Ziwa. Yeye mwenyewe anajieleza…**

Jina kangu ni Paulo Kusekwa, au niite MC paul. Napatikana Mwanza mjini. Mbali ya kuwa ni mshereheshaji lakini pia ni mjasiri-amali.



Nilianza kusoma vitabu kama burudani ya kawaida tu kwa sababu nilikuwa namuona mama yangu anapenda kusoma vitabu mba-limbali vya watunzi tofauti tofauti, lakini pia rafiki zangu wengi niliosoma nao tuliendana mawazo na tulipenda sana kukaa na kusimu-liana stori za kwenye vitabu.
Lakini baadae upenzi wa kusoma vitabu uliniongezea hamu ya kujifunza na kufungua mawazo yangu, na kupitia vitabu nimekuwa nikijifunza mambo mengi kuhusu watu na maisha kwa ujumla, na vinanisaidia kufikiri kwa mapana.

Kila kitabu kilinifundisha kitu kipya na kuni-fanya niielewe Dunia na baadhi ya mambo yake japo sio yote lakini angalau mengi na kwa undani zaidi. Kupitia usomaji wa vitabu angalau nayajua mambo ambayo nilikuwa siyajui. Usomaji umepanua mawazo yangu na kunijengea uwezo wa kufikiri kwa kina.
Mfano mdogo tu; katika ukurasa mmoja unaweza kupata faraja, maarifa, uzoefu, busara, hekima, ujasiri nk. Mambo ambayo huwezi kuyapata kirahisi ma-hali pengine.

Kama nilivyojitambulisha hapo juu, mimi ni mshere-heshaji (Master Of Ceremony) Kazi yangu inahusisha zaidi mawasiliano na kushughulika na watu, inahitaji mawazo mapana na maamuzi sahihi.
Usomaji wa vitabu umenisaidia kufahamu mbinu mpya za kazi, kuongeza ujuzi, maarifa, kuboresha lugha na namna ya kufikiri, kunijengea uwezo wa kuchambua na kutatua kwa utulivu changamoto zinazojitokeza kazini.
Hili ni jambo linalonifanya nifanye kazi yangu kwa ufani-si na kujiamini zaidi.

Mimi napenda kusoma vitabu vya motisha, mawasiliano na uongozi, sababu ni kwamba vitabu hivi hunisaidia kuongeza uelewa wa maisha, kuboresha namna ya kuzungumza na watu, na kunipa hadithi, methali na mifano ya kuvutia ninayoweza kuitumia wakati wa kuendesha matukio kama MC.
Lakini nitakuwa muongo mkubwa sana nikiacha kuvitaja vitabu vya riwaya za kijasusi vinavyohusisha upelelezi wa kutumia akili nyingi.

Kwa mwaka uliopita niliweza kusoma vitabu saba tu, japo si vingi sana lakini vilikuwa na mchango mkubwa katika kunikuza kifikra na kuniboresha ki-taaluma ndio maana sikutaka kujikita kwenye idadi tu, bali kuelewa na ku-tumia kile nilichokisoma, hasa katika kuboresha mawasiliano na kazi yangu kama MC.

Katika hili huwa ninajitengea muda wa shughuli zangu lakini pia ninajipangia ratiba yangu ya kusoma na hilo huwa nalimudu vizuri kwa sababu ni jambo lililo moyoni mwangu na ninalipenda sana.

Kusoma vitabu si adhabu bali ni uwe-kezaji binafsi, kila ukurasa una maarifa yanayoweza kubadilisha namna una-vyofikiri, kuongea na kufanya maamuzi, ukianza taratibu, hata kurasa chache kwa siku, utaona mabadiliko makubwa.

Ujumbe wangu kwa wapenzi wa Ngurumo ni kuwa waviangalie vitabu kama marafiki wanaokuongezea thamani, nawashauri wasome si kwa ajili ya wengine bali kwa ajili ya kujiboresha zaidi wao wenyewe.

---

**Ukihitaji huduma yake ya u-MC, kwa sherehe mbalimbali, hafla na program zingine, usisite ku-wasiliana na MC Paul. Popote Tanzania ataku-fikia na atakufanyia kazi iliyotukuka.**

**Wasiliana naye kwa Simu 0754976727 (call na Whatsapp)**

# MSALITI - 10

Na. Richard Mwambe



***Ilipoishia...***

**"Bila shaka ninyi ni wageni hapa, maana sura zenu tu ni ngeni kabisa. Unajua hapa Ngara tupo watu wachache, tunafahamiana kwa sura na sauti. Zaidi ni rafiki zetu kutoka Rwanda, Burundi, Uganda na wakati mwingine, hata wakongomani hujumuika nasi…"**

*Endelea…*

"Kwanini umesema mnajuana kwa sura na sauti?" Gina akadakiza swali.

"Hapa Ngara tuna vipofu watano wao hutujua sisi sote kwa sauti…" akajibu na wote watatu wakaangua kicheko.

"Na sisi tumetoka Mwanza," Amata akamjibu.

"Oh hahahahahaaaa… wasukuma nyie, safi, karibuni sana hapa Ngara," akasema kisha akapunguza sauti, "ila muwe waangalifu kuna watu wanawafuatilia, tena wamo humuhumu," akawaambia huku aniinuka na kuwaagizia bia mbilimbili. Akapotea zake nje ya baa ile.

"Wakati mwingine Mungu huwa anatuma malaika wake," Gina akasema.

"Ila kuna malaika wema na wabaya, tuondoke…" Amata akasema. Gina akatikisa kichwa kuwa wasubiri kidogo, Amata akatulia. Dakika kumi zilizofuata, Gina na Amata wakatoka kwenye ile baa. Mara baada ya wao kunyanyuka pale vitini na kuufuata mlango wa kuelekea nje, vijana wengine wanne nao waliinuka na kuelekea njia ileile.

"Tuna wasindikizaji," Amata akamwambia Gina huku akimshika mkono na kutoka nje kabisa ya ile Baa. Walipoyapita magari yaliyokuwa yamesimama hapo, Amata akamvuta Gina kifuani pake na kumkumbatia. Mabusu motomoto yalifuata huku akiwatazama wale vijana walivyokuwa wanagawana pande ili wawavamie.

"Wana mapanga kwenye makoti yao," Amata akamnong'oneza Gina huku akimshika vizuri. Aliziona silaha hizo kupitia miwani yake yenye uwezo wa kuona kitu cha chuma ulichokificha mwilini mwako. "Bastola zako zipo sawa?" akamuuliza.

"Yes!" Gina akajibu.

"Zipo silence?"

"Ndiyo,"

"Sasa huyo mwenye shati la drafti na yule mwenye nyekundu, hakikisha risasi yako inazama kifuani, hawa wawili niachie mimi…" Amata akamwambia Gina kisha akahesabu moja hadi tatu. Wakati huo wale vijana walikwishagawana tayari kwa shambulizi. Amata alipomaliza kuhesabu, Gina kwa wepesi wa ajabu aliinua mguu wake na kuchomoa bastola. Risasi mbili alizoachia zilifanya kile ambacho Amata alitaka. Watu wanne walianguka kwa tofauti ya sekunde tatu. Haraka Amata alivuta hatua hadi kwa mmoja wao na kumkandamiza kifuani kwa goti lake. Wale wengine alimwachia Gina ahangaike nao.

"Nani kawatuma mtufuatilie?" akamuuliza kwa sauti ya chini. Hakutaka kabisa kuvuta watu katika eneo lile. Goti lake lililokuwa juu ya kifua cha yule kijana lilimkandamiza sawasawa. Yule kijana pale chini alibaki akikoroma tu.

"Kkkkhhhuuummmjui.." akajibu kwa sauti ya kukoroma.

"Ndo nataka kumjua," Amata akamwambia. Yule kijana akakohoa mara mbili tu na kutulia kimya. Mikono ya Amata ikapita haraka kwenye mwili wa yule kijana na kuchukua kila alichoona kinamfaa. Akamchukua Gina na kuondoka zao kimyakimya. Yote hayo yakitukia, hakuna mtu aliyejua maana usiku huo kila mmoja aliye ndani alinogewa na starehe za humo.

Hatua za Kamanda Amata na Gina zikaishia kwenye ile nyumba ambayo Gina alielekezwa kuwa ndiyo ya Innocent Kabelwa. Wakaizunguka na kuhakikisha usalama upo wa kutosha. "Tunaingia wote au we unabaki nje?" Amata akauuliza kwa sauti ndogo. Gina akamjibu kwa ishara kuwa 'wote' wataingia ndani. Zoezi la wao kuingia liliwagharimu sekunde nne tu kwani ukuta ulioizunguka nyumba hiyo haukuwa mrefu sana. Uwa mpana uliwapokea. Ulikuwa uwa mtupu uliojengwa mabanda kadhaa yaliyoonekana labda kulikuwa na mifugo siku za nyuma. Amata akampa ishara Gina kuwa azunguke upande ule alioko na yeye angepita huu mwingine ili wakutane mbele ya nyumba hiyo. Wakafanya hivyo na dakika moja iliyofuata, wote wawili walitokea upande wa mbele kama walivyokubaliana. Ishara za kuashiria kuwa pande zote ni salama zikatawala. Amata akauendea mlango mkubwa huku Gina akiwa tayari na bastola mkononi kwa lolote. Alijidhatiti!

Funguo isiyoshindwa kitasa, ya TSA1 ilifanya kazi yake. Gina akachomoka pale alipo na kuingia ndani huku akimwacha Amata nyuma. Sekunde nyingine tatu wote walikuwa katika sebule kubwa iliyokuwa na viti vichache na Tel-

# MSALITI - 10



evisheni moja ya chogo ya kizamani ilikuwa hapo. Kwa mwanga wa kurunzi yenye ukubwa wa kalamu Amata alitembeza macho yake kidadisi mno huku Gina naye akifanya vivyo hivyo. Utulivu na utusitusi wa kiza ndani ya sebule ile vilitawala. Simu moja ya kizamani ilikuwa imepachikwa ukutani. Amata alipoiona akataka kuhakiki jambo.

Ni simu hii aliyotumia Besta? Akajiuliza.

Akaiendea na kuitazama kwa umakini. Alichotaka kujua tu ni kama ile ndiyo simu iliyotumika ama la. Akaingiza mkono mfukoni pake na kutoa glavu akavaa kwenye mkono wa pili kisha akainua ile simu kutoka kwenye kikalio chake. Akabofya namba za simu yake na kusikiliza nini kitatokea. Naam! Simu yake kutoka mfukoni ikapata mfurukuto. Akairudisha ile na kutoa simu yake akaangalia namba. Hakukosea, ni ileile. Amata alisisimkwa mwili.

Tupo eneo sahihi! Akawaza na kumpa ishara Gina kuwa waendelee vyumba vya mbele.

Wakiwa katika kumulika sakafu waliyokuwa wakiikanyaga ndipo walipogundua mburuzo wa kitu kupitia vumbi la sakafu ile. Walisita kuendelea na safari. Amata akakaza macho na kugundua matone kadhaa ya damu yakifuatana na mburuzo huo kuelekea kwenye vyumba vinavyofuata. Gina alijikuta kwenye hali ya hofu kuu. Alihisi mwili wake ukiingiwa baridi kila sekunde. Alitamani amwambie Amata watoke mle ndani lakini alishindwa. Amata alifungua chumba cha kwanza, hakuna kitu zaidi ya viroba vilivyotupwa huku na kule. Chumba cha pili nacho kilijawa makorokoro tu. Chumba cha tatu ndicho ambacho ule mburuzo uliingia na mlango wake ulikuwa wazi tu. Amata akamwonesha ishara Gina kuwa hapo ndipo kuna jambo.

Gina akaupiga teke na kuzidi kuufungua huku yeye akipita na kusimama upande wa pili wa muimo wa ule mlango. Hakuingia kabisa. Kitendo cha kuufungua ule mlango namna ile kilifuatiwa na muanguko wa kitu upande wa nyuma. Mwanguko ule ulimfanya Amata atulie kwanza, na Gina vivyo hivyo. Sekunde kumi zilizofuata hakukua na mjongeo wowote. Amata akavuta hatua taratibu na kuingia kwenye kile chumba. Kwa kutumia kurunzi zao walimulika huku na huko. Chumba kile kilikuwa tupu, hakuna kitanda wala chochote. Sakafu ilikuwa na damu iliyotapakaa hapa na pale. Jino moja lilikuwa chini na vidole vitatu vya binadamu. Mwili wa Amata ulisisimka. Akageuka na kumtazama Gina.

"Kuna mtu kateswa sana humu ndani mpaka kakatwa vidole na kung'olewa jino," akamnong'oneza Gina. Mwanamke huyo akaitika kwa kichwa. Ni pale alipomulika kurunzi yake nyuma ya mlango. Nini alikiona? Nguo ya jeshi ilikuwa chini, sakafuni. Aliinua uso na kutazama ule mlango. Palikuwa na henga ambayo labda ilining'inizwa ile nguo. Kwa kufungua kwa nguvu ule mlango ndipo ilianguka. Lakini kile kishindo, lazima kuna cha ziada! Amata akawaza na kumpa ishara Gina ya kutazama. Naam, lilikuwa vazi la jeshi, lenye mabaka mabaka. Koti la juu pamoja na suruali yake. Aliposhika na kuinua ndipo macho yake yaligongana na SMG iliyolala kimya huku ikiwa imesitiriwa na vazi hilo. Amata akatikisa kichwa juu chini. Akaanza kulipekuwa lile koti la jeshi katika mifuko yote. Hakukuwa na kitu zaidi ya karatasi moja ndogo. Ile karatasi ilikuwa imefinyangwa finyangwa. Amata akaitia mfukoni.


akamjibu. Kisha wakaondoka zao kama walivyokuja.

******************************

**Mpenzi msomaji, riwaya hii inakomea hapa. Ukitaka kuisoma unaweza kuinunua kwa Soft Copy Tsh 5000 na Hard Copy (Kitabu) Tsh 15,000.**

**Wasiliana nasi kwa Whatsapp 0766974865 ili upate nakala yako.**

**Asante kwa kuwa nasi!**



# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—10

**MTUNZI: ASHA SIRAJ**
**Whatsapp 0789044345**



**UTANGULIZI**

**Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhila**

***Ilipoishia…***

**Utashangaa au utakuja kuchukua vitu vyako, niliamini kweli dokta amekasirika hadi kuongea hivyo, nini nifanye ili arudi kwenye hali yake.**

***Endelea...***

Niliumiza sana kichwa changu nikitafakari namna ya kumfanya dokta atabsamu kama mwanzo. Basi, nilibeba mabegi yangu na yeye akawa amenisaidia baadhi ya vitu vilivyokuwa vimebaki kwenye gari.
Aliniomba nimfuate kwa nyuma. Baada ya kuzama ndani ndo nilizidi kushangaa zaidi na kusahau kama ameniambia nimfuate kwa nyuma, niliposhtuka sikuweza kumuona dokta mbele yangu.

Nyumba ile ilikuwa na vyumba vingi, kona za kutosha, hivyo sikujua chumba gani atakuwa ameelekea niliangaza macho yangu huku na kule ilibidi nitulie tu pale.
Baada ya kugeuka nyuma na bila kunikuta aliamua kunifuata na kunikuta nikiwa ukumbini nimesimama huku nikizidi kushangaa jinsi ukumbi ulivyokuwa mzuri.
"Shazma si nilikwambia unifuate nyuma mbona sasa umeganda na mabegi yako ukumbini?" aliniuliza.
"Samahani sana dokta!" niliomba samahani, akabaki kunitazama tu. Akaniambia tena nimfuate.
*Hebu Shazma acha ushamba!* Nilijiongela mwenye kisha nikapiga hatua kumfuata kwa nyuma. Tulifika ndani ya chumba kizuri kilichovutia kimuonekano. Ndipo mwisho wangu ulipoishia. *Hiki ndo chumba changu au?* Nilijiuliza mimi kama mimi baada ya kuliweka begi langu chini.

"Hiki ndo' kitakuwa chumba chako kuanzia sasa, ndani tupo wawili mimi na wewe tu ila kila siku huwa anakuja binti asubuhi na kuisafisha nyumba kisha jioni anaondoka hivyo utapata wakupiga naye *story* pale utakapo hisi upweke.
Kila kitu kipo humu, ukitaka kwenda kuoga kila kitu kipo humu humu hadi choo," aliniambia. Aisee lilikuwa bonge la chumba *uwwii* nini kingine nitake mimi.
Aliniambia nikimaliza kuoga nina uhuru wa kuzunguka kila mahara isipokuwa nje ya geti atatoka namimi pale nikiwa naenda *shopping* au kwenda sehemu ya mitoko fulani hivi.

Baada ya kuondoka nilijitupa kwenye kitanda, bonge la kitanda alafu sita kwa sita, analala mtu mmoja ni raha iliyoje nilikuwa nimezoea vile vitanda vya shule mtu hata pa kugeukia hapapo unahisi uKigeuka unaokotwa chini.

Nakumbuka sikuwa na simu ila judithi alianichia namba ya mama yake mdogo pindi nitakapo-m*miss* basi niombe simu na niweze kumtafuta ili tupate kuongea.
Nilibadilisha nguo. Yalikuwa majira ya saa nane kasoro mchana, kisha nilienda kuoga. *Washroom* palikuwa kama chumba kingine kwa ukubwa. Nilioga baada ya kumaliza nilibadilsha nguo. Ghafla sauti ya dokta ailisikaka akiniita kwenye mlango.

Nilivaa haraka kisha nikaenda kufungua mlango. "Kama upo tayari chakula kipo tayari tunaweza kwenda kupata chakula kwa pamoja" akanambia.
"Namalizia kisha nakuja," nilimjibu. Aliondoka. Basi mimi nilijipaka mafuta haraka na kujiangalia kwenye kioo cha kabati kama niko sawa au lah.
Baada ya kujiweka sawa niliondoka kuelekea sebuleni sehemu ya kupatia chakula maana kulikuwa na sehemu mbili; ukumbi mmoja ni kwa ajili ya kupata chakula na ukumbi mwingine ni kwa ajili ya kuangalia tivi na mambo mengine.
Basi niliketi kwenye kiti huku meza ilikuwa imejaa vyakula tofauti tofauti hadi raha. Ilikuwa unachagua kile ulicho kitaka wewe. Vyaku-

la vilikuwa vingi sana hadi nashindwa jinsi ya kuvitaja. Alikuja, naye akaketi pale.
"Shazma karibu chakula," alinikaribisha.
"Asante sana dokta, ila sidhani kama nitakula hicho chakula," nikamwambia.
"Kwanini Shazma? Hujakipenda?" aliniuliza.
"Hapana Dokta Shahdu ila nahisi kama bado una hasira na mimi, hivyo hata hamu ya kula sina" nilimjibu, "Naomba unisamehe sana kwa kile kilichotokea najua ni makosa yangu mimi, hadi wewe kutukanwa, ubishi wangu ndo umesababisha haya yote kutokea. Tafadhali naomba unisamehe sana," nilimuomba radhi. Shahdu alinitazama na kunijibu "Usijali Shazma, usiwaze kuhusu hilo, tule kwanza hayo sio ya kuzungumzia sa'hivi, tambua mimi niko sawa na nishasahau kile ambacho kimetokea leo," akanifariji.
"Hivi ni kweli au ndo unanipima ili nile ikiwa bado wewe moyo wako unahisi huzuni," nilimwambia.
"Shazma nishakwambia tayari kwa sasa niko sawa hivyo tunaweza kula na sitaki kuzungumzia kitu ambacho tayari nishasahau" akanijibu.


Basi, tulipata chakula, baada ya kumaliza kula nilitoa vyombo nakuweka meza sawa. Nlienda jikoni na kuosha vile vyombo, nilivifuta maji na kuvipanga kwenye kabati. Wakati huo dokta alikuwa mlangoni akinitazama hadi nilianza kujihofia kwani nina nini hadi dokta ananingalia hivyo, unajua mtu ukitazamwa sana unajikuta unawaza vingine.
Niligeuka na kutazama nguo yangu nilihofia wenda nikawa nimeingia *bleed* pasipo kujua.
Ila hapana nakumbuka nilikuwa na mda mfupi nimetoka. Hivyo haikuwa rahisi kuingia, sikujali niliendelea kusafisha pale nilipooshea vyombo, baada ya hapo nilifuta mikono yangu nakuelekea ukumbini.

Wakati TV ilikuwa wazi kuna *movie* ilikuwa ikionyesha pale. Ukumbini hapakuwa na mtu sikujua niwapi dokta ameenda.
Hivyo niliamua kukaa zangu nikawa naangalia *movie* pale. Muda kidogo dokta alikuja kukaa hapo ukumbini. Tuliangalia TV mpaka nikajikuta napitiwa na usingizi ukiweka na ule uchovu wa safari ndo kabisa.
Nilila sana, nilikuja kuamka mida ya saa kumi na mbili jioni. Nikamkuta dokta akiwa anacheza *game* kwenye TV, "Shazma umeamka?" akaniuliza.
"Ndio dokta kwa nini hujaniamsha mpaka sa moja hii?" nikamuuliza.
"Nilikuacha upumzike maana nimegundua umechoka," alinijibu.
"Ila unajua kabisa mpaka sasa hatujapika na mimi sijazoea kulala ovyo sijui ilikuwaje jamani mimi nikalala hivi!" Nilianza kujilaumu. Dokta akabaki anacheka tu pale, "kwa hiyo ndo ujilaumu hivyo jamani?"
"Haya bwana unanicheka kama nimefanya mazuri vile wakati huo ni uzembe moja wapo," nikasema.

Dokta ndo alizidi kucheka pale nakusahau kama alikuwa anacheza *game*, "*Ok* sintokucheka tena na kuhusu kupika usijali tayari nishaagiza chakula hivyo kipo njiani kinakuja," akanijibu.
"Ok, sawa!" Tuliendelea kupiga stori, nilitaka kumuona dokta akiwa anatabasamu sikutaka kumuona akiwa ameninunia.

Tuliletewa chakula pale, mida ya saa tatu usiku. Tulikula, baada ya hapo kila mmoja aliendа kupumzika chumbani kwake. Asubuhi yake dokta alikuwa anaenda kazini aliniomba nisije kutoka kwenda popote. Aliniaga na kuelekea kazini ila akuniacha pekee angu aliniachia na dada wa kazi aliyekuwa anakuja kufanya usafi na kuondoka jioni,.
Siku hiyo niliomba nipike mimi yeye afanye tu usafi, kama mnavyojua Shazma kwenye mapishi yuko vizuri *mashallah.*
Baada ya kumaliza kupata kifungua kinywa nilipumzika kidogo kisha nikaanza kuandaa chakula cha mchana, dokta alikuwa anatoka kazini jioni kama saa kumi na moja hivi. Alipenda sana kula chakula cha nyumbani.

Siku zilizidi kusonga mbele na miezi ikapita nikiwa pale kwa dokta, niliomba dokta ikiwezekana yule binti asije tena naweza kufanya usafi mimi mwenyewe... ***Itaendelea...***



**Katika nchi ya Baghdad kulikuwepo na kijana aliyejulikana kama Sinbad mbeba mizigo. Kijana huyu alijaaliwa kuwa na uwezo mkubwa wa nguvu za kuweza kubeba mizigo. Pia alikuwa na uwezo mzuri wa kiakili. Sinbad aliipenda sana kazi yake pia watu walimpenda kwa kuwa alikuwa akifanya kazi zake kwa umakini.**

Ilitokea sikumoja alipokuwa katika kituo chake cha kufanyia kazi alikuwapo mtu mmoja asiyemfahamu kabisa na kumpa kazi ya kupeleka mzigo wake sehemu husika. Mtu yule alitoweka baada ya kutoa maelekezo na kumpatia pesa yake. Sinbad baada ya kupewa maelekezo aliuchukuwa ule mzigo na kuanza kuukokota kwenye mkokoteni wake kuupeleka alikoelekezwa.

Njiani Sinbad alikutana na geti liliozungukwa na maua mazuri yenye kuvutia ndege, wadudu na wanyama kwa harufu na utamu wake. Sinbad alisimama kidogo eneo hili ili apate kushangaa uzuri ulioje wa eneo hili. Akilini alijiambia kuwa bila shaka ndani ya eneo hili kuna nyumba kubwa yenye bosi mkubwa.

Sinbad akiwa katika hali hiyo alituwa mzigo wake chini na kuanza kufuta jasho lake. Alisogea kidogo kwenye geti lile na kuona ndani kuna mambo ya kuvutia. Sinbad alikuwa ni kijana mwenye adabu na heshima lakini leo alisahau mambo yote hayo na akaanza kuchungulia ndani kwa watu. Alipokuwa hatoshelezi macho yake aliamua kuingia kwenye geti lile ili aone zaidi.
Sinbad hakuamini macho yake kama yanamuonesha sahihi, aliona nyumba kubwa yenye kila akijuacho kuwa kinahitajika, na aliona pia ambavyo havijui. Aliona nyumba iliyozungushiwa malumalu na lulu zikiwa zinaning'inia kama mauwa mazuri yaliyopambwa. Rangi za nyumba utadhani ni dhahabu iliyochovywa. Kwa hakika Sinbad alistaajabu sana. Kisha akaanza kuzungumza maneno yaloonesha kumlaumu mwenyezi Mungu kwa kuwapa watu wengine mali nyingi kama anazoziona pale. Pale aliendelea kumlaumu mwenyezi mungu kwa kumfanya yeye apate rizki kwa jasho jingi lakini watu wengine wapo wamekaa na bila jasho wanapata rizk.

Sinbad alilalamika sana hata akasikiwa na mwenye nyumba. Basi akaamrisha aletwe, akiwa natetemeka kwa woga Sinbad alipelekwa mbele ya Mkuu wa nyumba. Kisha akamwambia akae. Sinbad hakuamini kama meambiwa akae maana alifikiri atapewa adhabu kali. Basi mkuu wa nyumba akamuuliza "unaitwa nani kijana" "naitwa Sinbad" au Sinbad mbeba mizigo. Yule mzee akamwambia jina zuri sana na inaonekana wewe ni wajina wangu. Mimi naitwa Sinbad au ukipenda niite Sinbad wa baharini.

Baada ya kutambulishana majina Sinbad wa baharini akaanza kumwambia Sinbad mbeba mizigo. "kijana nimekusikia maneno yako, ila sio kosa lako kusema maneno yale na wewe pia si wa kwanza. Kwani wapo wengi wamesema kama wewe. Sasa leo nataka nikueleze kuwa mimi sikupata mali zote hizi kwa kukaa hapa bila ya jasho. Kabla sijapata mali hizi nilipata tabu kubwa sana na pengine hakuna anayeweza kunifikia jasho na taabu nilizopata wakati natafuta mali hizi"
Huu ni wakati sasa wa mimi kula na kuulia kwani mchumia juani hula kivulini. Kabla ya hapo mimi nilikuwa ni mfanya biashara wa majini yaani nasafiri visiwa mbalimbali. Utajiri wote kuu umetokana na taabu na mashaka yalonikuta. Nilisafiri safari SABA ambazo hizo nilipata taabu kubwa sana na sito sahau. Leo nitakueleza wewe na walokuwepo hapa yalonikuta kwenye safari hizo."

Basi kabla hajaanza kusimulia Sinbad mbeba mizigo akamwambia Mkuu mimi nina mzigo wangu natakiwa niupeleke sehemu hivyo niruhusu niondoke. Palepale Sinbad wa baharini akamwambia nitakupa mtu umuelekeze apeleke yeye hiyo mizigo na nitakulipa pato la siku yako yote ila ukae na mimi leo upate kusikia hadithi saba za safari zangu saba. Basi palepale akamuagiza mtu apeleke mzigo ule na vinywaji na vyakula vialetwa. Watu wakakusanyika na kukaa tayari kusikiliza hadithi za safari saba za sinbad. Basi bila ya kuchelewa akaanza kusimulia hadithi ya safari zake kama ifuatavyo:-

*Usikose toleo lijalo...*

**Je unafurahishwa na jarida letu?**

**Tuambie kupitia Whatsapp**

**+255 766 974 865**

SOMO KANIPONZA ni riwaya iliyoandikwa na mwandishi nguli wa fasihi ya Kiswahili Hammie Rajab miaka kadhaa iliyopita. Mwandishi huyu aliyetamba katika zama zake na manguli wengine ni mmoja kati ya walioacha urithi wa kifasihi katika Tanzania. Pamoja na kwamba magwiji wote wa fasihi waliopita wameacha urithi wa kifasihi hapa nchini lakini hapa tunazungumza kitu zaidi.

Hammie Rajab licha ya kuacha hazina ya maandishi bunifu ameacha pia urithi wa 'kipaji' kwa mmoja wa watoto wake ambaye ameasisi mradi wa kuyafanya maandishi haya bunifu kuwa hai na yanayotembea. Mohammed Hammie Rajab, mwandishi wa kitabu maarufu cha Maji Mandiga amekuja na mradi wa kutegeneza filam ya moja ya kazi za marehemu baba yake Mzee Hammie Rajab inayojulikana kama 'SOMO KANIPONZA'.

Mwandaaji mkuu wa filam hii Mohammed Hammie anaeleza kupitia akaunti maalum ya Somo Kaniponza aliyoifungua kupitia Instagram kuwa: Filam hii inafundisha jinsi tamaa ya muda mfupi na ushawishi wa watu wasiofaa unavyoweza kubomoa misingi imara ya heshima na uaminifu ndani ya nukta moja. Inatukumbusha kuwa usaliti hauangamizi tu ndoa, bali unaharibu utu, unavunja mahusiano ya kifamilia, na kukuacha ukiwa mpweke wakati dhoruba inapotokea, huku wale waliochochea anguko lako wakiwa wa kwanza kukucheka.

Somo Kaniponza si ya kwanza katika riwaya au vitabu vya Kiswahili kubadilishwa kuwa filam. Tangu miaka ya nyuma tumeona hadithi ya YombaYomba ilijulikana kama Fimbo ya Mnyonge ikibadilishwa kuwa filam. Zipo pia kazi za Ben Mtobwa ambazo zimefanywa filam na tamthiliya ya televisheni.

## 'SOMO KANIPONZA'
## HADITHI YA MAANDISHI INAYOTAKA KUTEMBEA

Kila shabiki wa mitandao ya kijamii hapa nchini au hata nje ya nchi atakuwa amekutana na mkululo wa matangazo ya filam hii ambapo tangu inaanza wazo mpaka inakamilika utengenezaji wake imekuwa ikiwekwa mitandaoni.

Utayarishaji wa filamu hii umefanyika katika mji wa kihistoria wa Bagamoyo na kuhusisha timu ya wasanii waliobobea kwenye tasnia ya uigizaji kama Madam Crista Komba na Bw. Maeda ambao wote wamewahi kuwa wakufunzi wa sanaa za jukwaani katika Taasisi ya Sanaa Bagamoyo, na wengineo kama mwanadada Hidaya Boli na Beatrice Taisamo. Deep Motion ndiyo wapo nyuma ya kamera wakibofya vitufe huku Chief Malalo akitafsiri vyema muswada huo kuwa picha inayotembea.

Filam hii inahusu maisha ya Mariam, mwanamke anayeishi na mumewe Abdi katika ndoa yenya furaha mpaka pale mimba yake ya kwanza inapoleta mtihani wa uaminifu. Baada ya daktari kuwapa onyo la kutokushiriki tendo la ndoa ili kulinda mimba hiyo changa, Mariam anajikuta katika ushawishi mzito kutoka kwa mtu ambaye alimwamini, Somo.

Lakini utofauti unakuja katika Somo Kaniponza ambapo inafanywa filam katika zama ambazo Tanzania imekuwa sana katika teknolojia ya 'dijitali' na habari. Tunategemea kuona kazi safi, HD, katika 'wide screen' ambayo bado tunasubiri taarifa kamili.

Ni matumaini yetu kuwa tutaiona filam hii kwenye majukwaa ya kimataifa likiwamo Zanzibar Iternational Film Festival. Kila la Kheri.



# Taha Hussein - Mkuu wa Fasihi ya Kiarabu na Busara ya Mwangaza

Na: Mervat Sakr


## Wasifu wa Akili Iliyoona Mwangaza

Imeandikwa na: Mervat Sakr

Taha Hussein hakuwa jina la kupita tu katika historia ya utamaduni wa Kiarabu, bali alikuwa tukio endelevu la fikra, akili iliyouasi ukimya, na mtu aliyeunda upya uhusiano kati ya binadamu, maarifa na urithi wa kitamaduni.

Alizaliwa Kusini mwa Misri mnamo mwaka 1889 katika mazingira duni na yenye upeo mdogo, kisha akapoteza uwezo wa kuona akiwa bado mtoto. Hata hivyo, upofu ambao kwa wengine ungeweza kuwa kifungo cha hatima, kwake uligeuka kuwa msukumo wa kipekee wa kuunda maono mapana zaidi; akili ikawa jicho lake la kwanza, na swali likawa njia yake ya kufikia ukweli.

Elimu yake ilianza katika *kuttab*, ambako alihifadhi Qur'ani Tukufu na kuipokea lugha ya Kiarabu katika umbo lake safi la mwanzo. Baadaye alijiunga na Chuo cha Al-Azhar, lakini haraka alihisi msongamano wa mbinu za elimu zilizotegemea kuhifadhi na kukariri, pamoja na kufunga mlango wa shaka na kuuliza. Pamoja na kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Kisasa cha Misri, Taha Hussein alipata anga tofauti, iliyoruhusu utafiti na mjadala, akafunguka kwa falsafa, historia na fasihi, na hapo mradi wake wa ukosoaji ukaanza kujengeka kwa utulivu na uthabiti.



Dalili za mradi huu zilionekana mapema katika tafiti zake kuhusu urithi wa Kiarabu, alipotoa vitabu kama *"Katika Ushairi wa Kijahili"* na *"Katika Fasihi ya Kijahili"*, kisha akapanua maono yake ya uhakiki kupitia *"Hadithi ya Jumatano"*, *"Kutoka katika Hadithi ya Ushairi na Nathari"*, *"Sura katika Fasihi na Ukosoaji"*, *"Mabishano na Ukosoaji"* na *"Ukosoaji na Mageuzi"*. Lengo lake halikuwa kuubomoa urithi wala kuudharau, bali kuuweka huru kutoka katika usomaji wa utakaso usiohoji, na kuuweka chini ya mbinu ya kisayansi. Ujasiri huu ulimletea mawimbi ya mashambulizi, marufuku na kesi za kisheria, lakini alibaki thabiti katika imani yake kwamba mwamko wa akili hauwezi kusimama bila uhuru wa kufikiri.

Mazungumzo yake na urithi yalikuwa mazungumzo hai na wahusika wake, si maandiko ya kimya. Aliandika kuhusu Abu Al-Alaa Al-Ma'arri katika "*Kuhuisha Kumbukumbu ya Abu Al-Alaa", "Pamoja na Abu Al-Alaa Kifungoni Mwake"* na *"Sauti ya Abu Al-Alaa"*. Pia alimjadili Al-Mutanabbi katika "*Pamoja na Al-Mutanabbi"*, na akasimama kwa tajriba za washairi katika "*Hafidh na Shawqi*", huku akipanua upeo wa usomaji katika *"Viongozi wa Fikra",* akitoa mifano ya uhakiki inayochanganya kuvutiwa na uchambuzi, bila kutukuza wala kubomoa.

Nchini Ufaransa, alikokamilisha masomo yake ya juu, Taha Hussein alikutana na mbinu za fikra za Maghalibi, na maono yake kuhusu utamaduni kama kitendo cha pamoja cha kibinadamu yakapanuka. Huko ndiko mawazo yake kuhusu elimu, utambulisho na ufunguzi wa ustaarabu yalipopevuka, mawazo yaliyojitokeza wazi katika vitabu vyake vya fikra kama *"Mustakabali wa Utamaduni Misri"*, *"Kioo cha Dhamiri ya Kisasa"*, "*Kioo cha Uislamu*", "*Kuiga na Kuhuisha"*, *"Kati ya Kati"*, "*Maoni Huru*" na "*Maisha na Harakati za Kifikra nchini Uingereza"*. Katika kazi hizi, alitetea dhana ya ufunguzi wenye ufahamu, akiona kuwa utambulisho haulindwi kwa kujifungia, bali kwa mazungumzo ya kina na ya kiuhakiki na dunia.

---

*-Kuttab - shule ya jadi ya Kiislam, elimu ya awali kwa watoto.*

**...akili pekee ndiyo huona yale ambayo macho hayawezi, na kwamba nuru ya kweli hutoka katika fikra jasiri, si katika uoni wa macho. *Taha Hussein***


# MY LIFE, MY PURPOSE – 02

UCHAMBUZI WA KITABU CHA RAIS MSTAAFU BENJAMIN MKAPA

**"MY LIFE, MY PURPOSE"**

**Na PROF. RWEKAZA MUKANDALA**

**{Imetolewa kutoka mtandaoni}**




## 2. KUZALIWA, MALEZI NA ELIMU

*Inatoka toleo lililopita…*

Aliunga mkono harakati za kupata uhuru kwa kuandika barua kwa Mhariri wa Gazeti la "Tanganyika Standard" ambalo sasa ni Daily News akiunga mkono hoja ya Uhuru. Barua ilichapishwa. Ila kijana Benjamini alitumia jina bandia!

Mhe. Mkapa alishinda mitihani yake ya kujiunga Chuo Kikuu Makerere, kwa kupata daraja la kwanza, akiwa kati ya wanafunzi watatu bora katika darasa la wanafunzi 51.

Makerere alikumbana na mambo mengi mapya: Alikuwa darasani na wanafunzi wa rangi tofauti, kwa mara ya kwanza alikwenda kucheza dansi ya kisasa, alipangiwa chumba cha kulala nk.

Mwamko wake wa kisiasa uliendelea. Alijiunga na Bodi ya Wahariri ya gazeti la "Transition"; alikuwa mwanachama hai wa kikundi cha wanafunzi cha TANU, akiwa katibu na hatimaye mwenyekiti wake. Alishiriki kwenye siasa za wanafunzi hapo chuoni. Aligombea Urais na ingawa hakushinda, wanafunzi wa kike walimpigia kura nyingi si kwa sababu alikuwa na rafiki wa kike, ila kwa jinsi alivyoweza kujieleza kuliko mpinzani wake. Alikuwa 'More articulate!' Aliteuliwa Makamu wa Rais wa Serikali ya wanafunzi, na hatimaye alikuwa mwenyekiti wa Baraza la wawakilishi la wanafunzi hapo Makerere. Alihitimu masomo yake Aprili 1962, miezi minne baada ya Tanganyika kupata Uhuru. Alipata shahada ya lugha na fasihi ya kiingereza na fonetiki. Alikuwa tayari kuifukuzia nia na ndoto yake.

## 3. MAISHA NA KAZI

Simulizi ya maisha ya utu uzima iko katika sehemu mbili. Kwanza ni alipoanza kazi mpaka alipogombea Urais. Pili ni maisha ya Urais. Sehemu hii ya simulizi imejaa sifa heshima na upendo mwingi kwa Mwalimu. Anastaajabu kwa jinsi Mwalimu alivyoiunganisha nchi katika kupigania vita vya ukombozi wa bara la Africa. Kama wazazi wake mzee Matwani na Bibi Nambanga walikuwa mashujaa wa sehemu ya kwanza ya maisha yake, hakika Mwalimu ndiye shujaa katika sehemu hii ya pili. Anamueleza Mwalimu kama labda alitumwa na Mungu kwa makusudi (Almost divine intervention).

Akiwa mtu mzima na mhitimu wa Chuo Kikuu Makerere Mheshimiwa Mkapa alipenda kuajiliwa kwenye Wizara ya mambo ya nchi za nje: Kwanza ilishindikana lakini, baadae akaambiwa, itawezekana kama ataajiriwa kwanza kama bwana shauri mkufunzi wa Wilaya, wakati akisubiri. Kwa hiyo aliajiriwa hivyo huko Dodoma April 1962.

Baada ya miezi minne August 1962 aliitwa Dar es salaam aende kujifunza udiplomasia Columbia Marekani.

Baada ya mwaka mmoja alirudi nchini akaajiriwa wizarani. Kazi yake kubwa ilikuwa kuchukua muhtasari wa mazungumzo Waziri wake au Mhe. Rais alipopata wageni. Anamsifia kwa ujasiri pale alipovunja uhusiano na Uingereza. Wakati huu Mhe. Mkapa alitumia muda wake binafsi ama kusoma habari Radio Tanzania Dar es salam, ama kumchumbia Bi Anna.

Siku moja aliambiwa anaitwa Msasani kwa Mwalimu. Walipaita Msasani nyumbani kwa Mwalimu "The Clinic". Mwalimu akamwambia anamteua kuwa Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Nationalist. Ilibidi aende Uingereza kujifunza mambo ya magazeti kwenye magazeti ya The Mirror.

Alirudi na kuanza kazi chini ya Mwalimu kama Mhariri Mkuu, Mhe. Mkapa alikuwepo Arusha wakati wa Azimio mwenzie Nsa Kaisi ndiye aliyebuni neno la Arusha Declaration, walilitumia kwenye The Nationalist, Mwalimu akalipenda, basi hayo maamuzi yakaitwa hivyo.

*Itaendelea...*



Katika Mwaka wa NNE wa NGURUMO: Mwasisi wa Jarida hili alipokea Tuzo ya Heshima ya Fasihi ya KISWAHILI kutoka TAFF. Tuzo hii ililetwa kupitia Jarida la NGURUMO.



Katika Mwaka wa NNE: Hii ni moja ya picha inayomwonesha Majid Mswahili akikabidhi kitabu hicho kwa balozi wa Tanzania Nchini Ujerumani. Ni katika moja ya matukio ya KISAWHILI



Katika Mwaka wa NNE wa Ngurumo: Mwandishi Maundu Mwingizi aliibuka mshindi wa kwanza katika Tuzo ya Mwalimu Nyerere msimu wa 3. Hii ni moja ya picha KUBWA iliyopamba moja ya toleo letu



Katika Mwaka wa NNE wa Ngurumo: Ulikuwa ni mwka wa kubadilishana maarifa. Waandishi; Anna Mbise kulia na Dotto Rangimoto 'Jini Kinyonga'

Hizi ni PICHA chache tu ambazo zilichapishwa kwenye majarida yetu mbalimbali ya mwaka wa NNE yaani kati ya toleo la 36—48.

Tunakushukuruni nyote kwa kuwa pamoja nasi. Basi shime kwa mwaka wetu wa TANO tuwe pamoja kama dawa.

TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.
Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.
Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com

## PONGEZI KWA NGURUMO

Pongezi zetu twatoa,
Ngurumo nyote pokea,
Hamasa kubwa mwatutia,
Uandishi kuupenda.

Waandishi mwatusogezea,
Na wapenzi wa fasihi mwatuletea,
Makala mwatuandikia,
Mwatufungua akili.

Arobaini na nane toleo,
Si la jana wala leo,
Ngurumo ni kichocheo,
Kwa fasihi Tanzania.

Kweli mwatueleimisha,
Kwa utamu usiokwisha,
Kusoma mwatuhamasisha,
Ujinga unatuondoka.

Hadithi mwahadithia,
Na malenga twajisikia,
Habari mwatupatia,
Na burudani kedekede

Twawapa nyingi kongole,
Mwanzo wa ngoma ni lele,
Twayatabiri ya mbele,
Ngurumo mtaja tisha.

Hongera kwenu watozi,
Kwa hekima nyingi hizi,
Mwatunyima usingizi,
Ngurumo kulisubiri.

**Pongezi kwa Ngurumo**

## WAPE WATU WATU WAO

Siwafiche abadani
Kwani hao ndugu zao
Ni kweli na si utani
Wengi wao wana wao
Kama wataka amani
Basi, wape watu watu wao

Usichengechenge kona
Hapo kuna wana wao
Macho machozi kutona
Hawaoni umbu zao
Sipojali utaona
Kivumbi na jasho lao

Chuki wakuchukia
Walilia damu zao
Laana wakutupia
Wakidai haki yao
Kwanini wapuuzia
Kwani ni ujinga wao?

Waapa kuparandana
Kuziacha nyumba zao
Wasema watandamana
Watamwaga damu yao
Yanini kusakamana
Wape watu watu wao

Mimi nimemaliza
Nimekwambia mwanao
Ninaomba sikiliza
kilicho kilio chao
Kabla hujawacharaza
Wape watu watu wao.

**Shujaa Maneno**
**Bagamoyo kwetu**

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE NAKALA YAKO
DAR ES SALAAM
Duka la Kona ya Riwaya
Kinondoni Morocco
Simu:
0655428085
Zammira


KAMANDA AMATA
MSALITI
"Kamwe hatoki upande wa adui yako"
MSALITI
15,000/=
Kona ya Riwaya
BOOKSHOP
Fika dukani kwetu au wasiliana nasi Kwa Simu
0655 428 085
Mliopo mikoani tunakutumieni.


KINAPATIKANA
ARUSHA
Kinapatikana Kwa Ally Said Shaban, nje tu ya KIMAHAMA Bookshop
Simu: 0757690302 na 0656744390
KAMANDA AMATA
MSALITI
"Kamwe hatoki upande wa adui yako"
15,000/= tu
Jipatie Nakala Yako Sasa!


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE NAKALA YAKO
ARUSHA
Nje ya Duka KIMAHAMA
Simu
+255 757 690 302
ALLY SAID

# KUTOKA MAKTABA
# MWANDISHI WA ENZI HIZO: 2. AGORO ANDURU (02)

**AGORO ANDURU - Machache yamhusuyo**

**1. Mwandishi wa Tanzania**

Agoro Anduru ni mmoja wa waandishi waliochangia katika ujenzi wa fasihi ya Tanzania, hususan katika kipindi ambacho waandishi wengi walikuwa wanaandika kwa Kiswahili. Lakini yeye pekee alikuwa akitumia pia Kiingereza.

Anatajwa katika tafiti nyingi za fasihi kama sehemu ya waandishi waliounda kile kinachoitwa:

“Bilingual Literature of Tanzania”

— fasihi inayojengwa kwa kutumia lugha zaidi ya moja.

**2. Maudhui ya Uandishi Wake**
Kazi zake nyingi huwa zinagusana na:

Maadili ya jamii

Migongano ya kisiasa

Maisha ya kila siku


Mabadiliko ya kijamii

Haki na utu

Hivyo anahusishwa na kundi la waandishi ambao wanatumia fasihi kama njia ya kuonesha ukweli wa jamii.

**3. Kazi Alizowahi Kutajwa Kuzifanya**
Ingawa si mwandishi “mainstream” kama kina Kezilahabi au Habwe, ametajwa mara kadhaa katika tafiti na makala za kitaaluma kama mmoja wa waandishi walioweka michango yao katika short stories na creative writing za Kiingereza nchini.

Baadhi ya maeneo anayotajwa sana ni:



AGORO ANDURU

Hadithi fupi (short stories)

Makala za kijamii

Uandishi wenye msimamo wa haki

**4. Kwa nini jina lake halisikiki sana?**
Sababu kuu ni kwamba: Alikuwa mwandishi wa kipindi ambacho fasihi ya Kiingereza haikuwa maarufu Tanzania. Kazi zake nyingi zilikuwa katika majarida na machapisho ya kitaaluma, si vitabu vya kibiashara. Hakuwa na uendelezaji mkubwa wa kazi zake kibiashara.

Hata hivyo, jina lake lipo kwenye vielelezo vya wanafasihi kama miongoni mwa waandishi wa mwanzo waliotumia Kiingereza kwenye uandishi bunifu hapa Tanzania

**Vitabu/Makusanyo vya Agoro Anduru**

**This Is Living: And Other Stories** — jumla ya hadithi fupi kwa Kiingereza.

**Temptation and Other Stories** — mkusanyo wa hadithi fupi, iliyoandikwa miaka ya mwanzo ya 1980s.

**A Bed of Roses and Other Writings** — mkusanyo mwingine wa kazi zake.

**Kukosa radhi** — novella kwa Kiswahili, ikiwa ni mfano wa uandishi wake wa Kiswahili.

Inawezekana pia kuna makusanyo au hadithi zilizosambazwa kupitia magazeti — jambo ambalo limekuwa changamoto kwa uhifadhi wa vitabu hivyo.

**Changamoto ya upatikanaji wa machapisho yake**
Kwa mujibu wa makala ya utafiti wa fasihi, kazi zake ni miongoni mwa “kazi za mapema” za fasihi ya Kiingereza nchini Tanzania — hivyo si kila kazi imechapishwa tena au sasa inapatikana kirahisi.

Makusanyo kama “Temptation and Other Stories” na vingine vinaweza kuwa vigumu kupatikana kutokana na muda mrefu na uhifadhi duni.

Kazi ya Kiswahili kama “Kukosa radhi” inaashiria kwamba Anduru alikuwa ameamua kuandika kwa Kiswahili pia — si tu Kiingereza — jambo ambalo linaongeza thamani kwa fasihi ya Tanzania.

## SAFARI YA MALEZI 8: MITINDO YA MALEZI

**SAFARI YA MALEZI 8: MTINDO BORA WA MALEZI NA UTEKELEZAJI WAKE**

### 7.0 Mtindo Bora wa Malezi

Baada ya kuangalia mitindo mbalimbali ya malezi, ni muhimu kuelewa ni nini kifanyike ili kujenga mtindo bora wa malezi unaozingatia mahitaji ya mtoto na mazingira anayokulia. Mtindo bora wa malezi hauko upande mmoja tu wa nidhamu kali au uhuru usio na mipaka, bali ni mchanganyiko wa mbinu zinazolenga kumlea mtoto kwa upendo, mwongozo, na uwajibikaji. Lengo kuu la mtindo bora wa malezi ni kumsaidia mtoto kukua akiwa na maadili mema, uwezo wa kufanya maamuzi sahihi, kujiamini, na kuheshimu wengine. Katika mada hii, tutaangazia vipengele muhimu vinavyomsaidia mzazi au mlezi kujenga malezi bora katika maisha ya kila siku.

### 7.1 Vipengele vya Mtindo Bora wa Malezi

#### 7.1.1 Mawasiliano ya Wazi na Yenye Heshima

Na. KELVIN JOHN KYARA

0753767930





Mawasiliano ni msingi muhimu sana katika kujenga mtindo bora wa malezi. Mzazi anapowasiliana na mtoto wake kwa uwazi na heshima, humsaidia mtoto kuelewa matarajio, mipaka, na sababu za maamuzi yanayofanywa. Mawasiliano bora yanahusisha kumsikiliza mtoto kwa makini, kumpa nafasi ya kueleza mawazo na hisia zake, pamoja na kumwelekeza kwa lugha inayoeleweka kulingana na umri wake.

Katika malezi bora, mawasiliano hayapaswi kuwa ya kutoa amri pekee, bali ya kujenga maelewano na uelewa. Faida ya mawasiliano ya wazi ni kujenga uhusiano wa karibu na wa kuaminiana kati ya mzazi na mtoto. Mfano, mzazi anapozungumza na mtoto kuhusu tabia isiyofaa kwa utulivu na kumweleza madhara yake, mtoto hujifunza kosa lake bila kujenga hofu, chuki, au uasi dhidi ya mzazi.

#### 7.1.2 Nidhamu Yenye Upendo na Usawa

Nidhamu ni sehemu muhimu ya malezi bora, lakini inapaswa kutolewa kwa upendo, haki, na busara. Nidhamu haimaanishi adhabu kali au mateso, bali ni mchakato wa kumwelekeza mtoto kutambua tofauti kati ya lililo sahihi na lisilo sahihi. Sheria na mipaka vinapaswa kuwekwa wazi, kueleweka, na kusimamiwa kwa uthabiti bila upendeleo.

Faida ya nidhamu yenye upendo ni kumjenga mtoto anayeheshimu sheria na kuwajibika kwa matendo yake. Mfano, mtoto anapokiuka kanuni ya nyumbani, mzazi anaweza kumpunguzia muda wa michezo au kumpa jukumu la ziada la nyumbani ili ajifunze uwajibikaji, badala ya kutumia adhabu kali zinazoweza kumuathiri kihisia au kimwili.

#### 7.1.3 Kutoa Mfano Bora wa Tabia na Maisha

Mzazi au mlezi ni mfano mkubwa kwa mtoto. Watoto hujifunza zaidi kwa kuangalia na kuiga tabia za wazazi wao kuliko kusikiliza maelekezo ya maneno pekee. Hivyo, mzazi anapaswa kuonyesha tabia anazotamani mtoto awe nazo, kama vile uaminifu, heshima, bidii, nidhamu binafsi, na kuwajibika katika majukumu ya kila siku.

# ELIMU JAMII

Mfano, mzazi anayeheshimu muda, kutimiza ahadi zake, na kuonyesha heshima kwa wengine humfundisha mtoto maadili hayo kwa vitendo. Mtoto anayekua katika mazingira yenye mifano mizuri hukua akiwa na tabia njema na mtazamo chanya kuhusu maisha.

**7.1.4 Upendo na Msaada wa Kihisia kwa Mtoto**

Upendo ni nguzo kuu ya mtindo bora wa malezi. Mtoto anayepata upendo na msaada wa kihisia hukua akiwa na kujiamini, utulivu wa kihisia, na uwezo wa kukabiliana na changamoto za maisha. Upendo huonyeshwa kwa maneno ya faraja, kusikiliza matatizo ya mtoto, kutumia muda wa pamoja, na kumtia moyo anapokosea au kushindwa.

Mfano, mtoto anaposhindwa katika masomo au michezo, mzazi anayemfariji na kumsaidia kutafuta njia ya kuboresha humjenga mtoto anayejifunza kutokana na makosa badala ya kukata tamaa au kujiona hafai.

**7.1.5 Ushirikiano kati ya Familia, Shule na Jamii**

Mtindo bora wa malezi hauishii nyumbani pekee, bali unahitaji ushirikiano wa familia, shule, na jamii kwa ujumla. Mtoto anapopata mwelekeo unaofanana katika mazingira haya yote, hukua akiwa na uelewa mzuri wa mipaka ya kijamii na wajibu wake katika jamii. Ushirikiano huu husaidia mtoto kukuza maadili mema, nidhamu, na heshima kwa wengine.

Mfano, mzazi anayeshirikiana na walimu kufuatilia maendeleo ya mtoto shuleni humsaidia mtoto kuelewa umuhimu wa elimu na uwajibikaji.

**Hitimisho**

Kwa ujumla, mtindo bora wa malezi unahitaji uwiano kati ya nidhamu na upendo, uhuru na mipaka, pamoja na mawasiliano ya wazi. Malezi bora ni safari endelevu inayohitaji subira, uelewa, na kujifunza kila siku. Malezi haya huweka msingi imara wa kumjenga mtoto anayewajibika sasa na kuwa mtu mzima mwenye mchango chanya katika familia na jamii hapo baadaye.

# SHUBAKA LA VITABU

***Inatoka Ukurasa wa 18...***

Upande wa kibinadamu wa tajriba yake ulijitokeza kwa uzuri mkubwa katika kitabu chake maarufu *"Al-Ayyam (Siku)"*, ambacho hakikuwa wasifu wa kawaida, bali ushuhuda wa kina wa kibinadamu juu ya mapambano ya akili dhidi ya umaskini, ujinga na upofu, na simulizi la kizazi kizima kilichoamini kuwa elimu ndiyo njia pekee ya ukombozi.

Sambamba na wasifu, aliandika riwaya na hadithi, akiacha kazi kama *"Dua ya Korongo"*, *"Mti wa Taabu"*, *"Bustani ya Miiba"*, *"Upendo Uliopotea"*, *"Ahadi ya Kweli"*, *"Walioteswa Duniani"*, *"Ndoto za Shahrazad"*, *"Jumba Lililorogwa"*, *"Bustani ya Wanyama"* na *"Shule ya Ndoa"*, ambako hisia ya kijamii ilichanganyika na mwelekeo wa kimaadili na kibinadamu ambako hisia ya kijamii ilichanganyika na mwelekeo wa kimaadili na kibinadamu.

Maslahi yake katika historia na fikra za kidini hayakutengana na mradi wake wa ukosoaji. Aliandika *"Pembeni mwa Wasifu wa Mtume"* na *"Fitna Kuu"* katika juzuu zake mbili: Uthman na Ali na Wanawe, akitoa usomaji wa kiakili wa matukio ya msingi katika historia ya Kiislamu, mbali na simulizi za kimapokeo na mihemko ya kimadhehebu.

Taha Hussein pia aliamini katika umoja wa utamaduni wa kibinadamu, akajifungua kwa tafsiri, na kuhamishia katika Kiarabu kazi za fasihi na fikra za dunia kama *"Oedipus na Theseus"*, *"Andromaque"*, *"Zadig"*, *"Mfumo wa Waathene"* na *"Roho ya Elimu"*. Pia aliandika *"Kutoka Fasihi ya Tamthilia ya Kigiriki"*, *"Kutoka Fasihi ya Tamthilia ya Magharibi"* na *"Makala Teule kutoka Ushairi wa Tamthilia ya Kigiriki"*, akisisitiza kuwa fasihi ya kibinadamu ni mto mmoja wenye vijito vingi. Aidha, alichangia kufufua urithi kwa kuhakiki "Kalila na Dimna", akiunganisha kati ya jana na leo.

Taha Hussein alifariki dunia mnamo mwaka 1973, lakini aliacha nyuma urithi hai wa fikra na neno, unaotufundisha kwamba akili pekee ndiyo huona yale ambayo macho hayawezi, na kwamba nuru ya kweli hutoka katika fikra jasiri, si katika uoni wa macho.

## HAPPY NEW YEAR '13'—Twahir Yusuph

***Ilipoishia...***

***Alilia mno akiwa chumbani kwake juu ya kitanda, nyumbani kwao. Ni zaidi ya unyama, uliofanywa na muuaji huyo ambaye alishalitaja jina lake kuwa ni Wizard Gaino.***

---

*Endelea…*


Baada ya dakika kadhaa kishindo cha nguvu kikasikika, ni yeye Wizard Gaino alilitupa shoka lake pembeni huku akilia, bado aliendelea kumtaka Labi aseme kwanini walimbaka mwanawe? Kwanini walimtendea unyama kama ule binti yake? Hakuna wa kumjibu, tayari Labi Kimati alishatorokwa na roho yake, ulibaki mwili tu usiotamanika. Punde akanyamaza Wizard, macho yake yenye picha ya hasira kali yakaitazama kamera. "Najua askari wenu washafika hapa kuja kuuchukua huu mzigo wenu ili mkaufukie." aliongea akitabasamu, machozi bado yakimchirizika. "Hey rafiki zangu, mimi nimeshamaliza kilichonifanya nisilale vizuri hii miaka minne niliyotengana na nyinyi, sasa nipo huru." aliongea akiitanua mikono yake.

"I AM FREEEEEEEEEE, NIPO HURU SASA." Alipaza kelele kwa nguvu na kucheka kwa sauti ya juu huku akiangaza usowe darini pia, ilhali akiendelea kuitanua mikono yake. "My Heart is free now, even my life is free, freee, freeeee, HAPPY NEW YEAR GENTLEMEN." Aliongea akiitazama tena kamera, mara punde kiza kikatawala kwenye kila kioo cha simu cha aliyekuwa mubashara akilitazama tukio hilo liliowasisimua wengi. Tayari askari walishawasili eneo ambalo wataalamu walipadukua, sehemu ambayo paliwapa alama kuwa muuaji Wizard Gaino anapatikana hapo. Inspekta Azizi Kasese ndiyo aliliongoza kundi hilo la maafande.

Aliwatawanya wenziwe na kuizunguka nyumba hiyo kuu kuu waliyoikuta porini hapo, kwa tahadhari zote wakaanza kuisogelea kwa hatua za uangalifu wa hali ya juu. Waliifikia, mbele ya mlango dhaifu wa nyumba hiyo mbovu, askari wakiwa na mitutu yao iliyotazama mbele kwa tahadhali na umakini, Inspekta Azizi Kasese akisimama katikati aliupiga teke mlango huo na kuwafanya askari polisi walio pembe zote kuzama ndani kwa kasi na uangalifu mkubwa. Viganja vyao vikiwa kwenye vitufe vya kuiamuru risasi isafiri, midomo ya mitutu waliyoishikilia ikigeuka kila kona ndani humo, macho yao yalifanikiwa kuona samani nyingi zilizochakaa, vitu vilivyozagaa hovyohovyo, pamoja na kiroba kilichozungukwa na kutapakaa damu nyingi mno.

Ndiyo, kama kawaida ya muuaji, alifanya vilevile kama kwa Jax na Imraan, leo ikiwa ni zamu ya Labi Kimati. Mwili wake ulikusanywa ndani ya kiroba, kichwa kikiwa pembeni kinaonekana, yeye Wizard Gaino akiwa hayupo. Ulikuwa msiba mwingine mkubwa, uliokuja na majibu ya misiba yote iliyopita, ambayo ilitokea kwa mtindo kama huo wa kikatili. Kilikuwa KISASI, muuaji alikuwa akilipa deni la ubaya alilowahi kukopeshwa na familia hizo kubwa nchini Takaseni, leo alilimaliza. Wakiwa kwenye ofisi zao CDF Rashidi Koboko na IGP Edward Kituo, fedheha ziliwakumba, mioyo yao ilinyong'onyea, walichoka.

Bwana Kimati Sesewa hakuna alichoweza kufanya akiwa kwenye kasri lake zaidi ya kumwaga machozi tu. Inspekta Kasese pamoja na askari wake, kitu pekee walichofanikiwa kukipata ni mwili wa marehemu uliohariibiwa vibaya mno, lakini sio muuaji bwana Wizard Gaino. Alishatoweka tayari.




* * *

Jua na mbalamwezi havikuchoka kupishana,

siku mbili zikapita tangu litokee tukio lile, CDF Rashidi Koboko pamoja na IGP Edward Kituo wakatangaza kujiuzulu kwenye nafasi zao. Rais wa nchi ya Takaseni akateua warithi wao. Pia akatangaza kufanyika uchunguzi wa kesi hiyo ya miaka minne nyuma iliyopita, inayomhusu Mona binti yake Wizard Gaino. Uchunguzi ulifanyika haraka, shahidi alikuwa moja ya vijana waliotekeleza adhma ya kumteka na kwenda kumtupa Wizard Gaino baharini, alijisalimisha mwenyewe, alieleza kila kitu. Aliyekuwa CDF Rashidi Koboko, IGP Edward Kituo, pamoja na tajiri Kimati Sesewa walikutwa na hatia, wote watatu wakahukumiwa kifungo cha Maisha gerezani. Yote hayo yalisimamiwa na Inspekta AZIZI KASESE, kwa kushirikiana na askari wengine.

Zile siku tisa alizopewa hazikuisha, kesi aliyokabidhiwa ikawa tayari imetamatika. Muuaji hakupatikana, ila wahusika wa sababu ya mauaji yale walishikwa. Wiki moja mbele, ule ukurasa wa kifo ukaweka chapisho la ki'maandishi na picha ya mwewe aliyezichanua mbawa zake akiwa angani, huku maandishi hayo yakisomeka. "HAPPY NEW YEAR MY LIFE"

TAMATI

**Inatoka uk. Wa 10. Kamba za Masai**

Wakafanya Kazi kwa Bidii Kila Mmoja Akitaka Kuonyesha Kuwa ni Bora Kuliko Mwingine. Wakasahau Malalamiko Muhimu, Wakajiktा Kwenye Kubaguana. Mtifuano Ulikuwa Mkubwa Mno. Mimi na Amitha Tulikuwa Kama Chui na Simba. Hatupatani. Kila Tulipokutana, Vita Baridi Iliwaka. Nilipinga Matamko Yake, Akayapinga Yangu.

Baada ya Kazi, Tulikutana Chemba. Tukacheka na Kuwasha Winston SM na Kuvuta Kiroho Safi.

Ndipo Baada ya Kampuni Kukaa Sawa Kifedha, Boss Wetu Alitoka na Kutusihi Sana Tusibaguane Bali Tujenge Familia Zetu Plus Nchi. Mwisho Kabisa Aliahidi Kuweka Mambo Sawa. Na Baada ya Mambo Kukaa Sawa, Mimi Kama Kata Ndombe na Amitha Tuliitwa Jukwaani na Kupatanishwa. Maisha Yakasonga.

Hii Ilikuwa ni 1974 Pale Bombay.

*Tunaposoma vitabu, tunapata mawazo, dhana na maarifa tofauti ambayo hutusaidia kufungua fikra za kuondoa changamoto za kijamii zinazotuzunguka. Halikadhalika, hutuwezesha kuona na kufungua tija mbalimbali za kimafanikio ndani ya changamoto zinazotukabili. Unaposoma—hisia humezwa na akili katika kung'amua na kuamua mambo. Kitabu ni zawadi.*

Dr. Gervas Kasiga—FB Disemba 12, 2025



# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (08)- Na: Eva Mrema

***Ilipoishia…***

***Siku hizi wenye ndevu zao, wanadanga kuliko wanawake na mbaya zaidi ni kwamba wao wanajua kuwa mna shauku sana na ndoa. Jihadharini. Mchungaji naomba unisamehe" alihitimisha kusema hayo mwanamama yule na kutoa cheti cha ndoa kwenye mkoba wake. kuwekeza wazazi wangu wakati wa uhai wao.***

*Itaendelea...*

Niliweka mazingatio kwenye kubadilika kwa maisha yangu binafsi. Nilipopata kazi nikaanza kuwekeza na sasa nusu ya nilivyopoteza ninavyo"

Sunche alinifuta machozi yaliyonitiririka mashavuni akanipa pole na kunikumbatia kwa kitambo.

Alinishika mabega na kuuvuta mwiliwe nyuma kutoka kwenye kumbatio. "Sikiliza! Mimi na wewe tutakula yamini, tutaapa kiapo cha damu, sitaki kukuacha hata ndotoni. Siombei uniache hata baada ya kìfo changu, 'your my soul mate' Tabita" Sunche alinena hayo huku kayashika mashavu yangu kwa viganja vya mikono yake na kunitazama machoni kwa hisia kali.



Nilitarajia maswali na hukumu nyingi kutoka kwa Sunche; pengine kwa sababu masikio yangu yalizoea kelele za kejeli kutoka kwa kila aliyeijua hadithi ya mimi na Pharao. Kwa Sunche haikuwa hivyo. Machozi yalinipungua kwa haraka baada ya kuona kwa mara ya kwanza kuna mtu kanielewa katika kutokueleweka kwangu.

Alinikumbatia tena Sunche wangu. Aliibusu shingo yangu na hapo mtomasano ukashika hatamu.

Tulijikuta ndani ya dimbwi la huba zito. Penzi lake liliulainisha moyo na mwili wangu. Nilijihisi wa pekee na muhimu mara zote. Sikuwahi kujua kabla kama kupendwa humaanisha hivi. Sunche aliniweza bwana! Hakuna ufa hata mdogo aliouacha moyoni mwangu. Aliivaa ratiba yangu na kuwa msimamizi. Alihakikisha nakula na kunywa kwa wakati. Mazoezi yalisalia ya kawaida na mwisho wa juma tulifanya pamoja.

Jambo moja lilinitatiza na kuniweka katikati ya damu yangu na wa ubani wangu. Ilinichukuwa muda kumtambulisha Sunche kwa mdogo wangu na hii ni kutokana na uhalisia wa husiano langu lililopita. Nilifunga roho na kujivisha mabomu. Kama nilivyotarajia, dogo hakumkubali, moyoni alihisi na mara hii nitaangukia pua. Alionesha chuki za wazi kwa Sunche, nashukuru Sunche alikuwa muelewa. Alijitahidi kumuweka karibu kwa akili na upendo mkubwa. Ilichukua muda na gharama kujithibitisha ila mwishoni mdogo wangu akaanza kuwa muungwana kwa Sunche. Ukaribu wangu na Sunche ni zaidi ya ule wa chupa ya soda na kizibo chake. Alipo, kama sipo, basi ujue ni kazini. Mimi na yeye tulitamatisha mwaka wa uhusiano wetu.

Tulifurahiana bila kuchokana, wakati huu tayari nilitayarika kuhusu swala la ndoa.

Sitaki nataka naye mtu jamani, niliitamani ndoa ili niwe rasmi ubavu wa Sunche. Niliiogopa ndoa shauri ya hofu ya kutelekezwa siku ikiwadia. Si hivyo tu! Hadithi za magumu ya ndoa nazo zilishamiri, zilivunja sana moyo. Nilibembea; kulia hofu ilinilemea, kushoto huba lilinikolea. Sunche alilibaini hilo mapema sana. Hakuacha kusisitiza namna ananipenda, nami nilimuamini kupita hilo neno lenyewe.

SURA YA TANO.

Tulipanga safari ya kwenda Tanga kutalii, ulikuwa msimu wa likizo kwa Sunche na mdogo wangu, vyuo vingi vilifungwa. Binafsi niliomba ruhusa ya siku tano kazini. Siku ya safari haikukawia, kama utani ikawadia. Safari ilikuwa ya utulivu na vituo vingi vya mapumziko. Kila tulipojisikia tulipaki gari na kuweka kambi. Tulikula, kunywa na kuufurahia wakati wetu pamoja. Tulisonga na hatimaye tuliwasili Tanga mchana wa siku ya pili. Hatukwenda japo karibu na pahala lilipo chimbuko la


**RIWAYA: NGUVU YA KIAPO**

Inapatikana katika kitabu (nakala ngumu) na soft copy (nakala tepe) kwa bei ya kirafiki.

**KITABU** - Tsh 10,000
**Dar es salaam:**
- Duka la Kona ya Riwaya - 0655428085
- Kalamu Tulivu Magomeni - 0718975659
- Posta Mpya kwa Joji - 0713454152
- Temeke kwa Eva Mrema - 0742630141

Soft Copy (Nakala tepe) PDF - Tsh 5,000
'Offer' kupitia Ngurumo ya Mwandishi ni - Tsh 3,000
Lipa kwa **MPESA LIPA NAMBA 36499709 Eva John Mrema**

asili ya mama yangu, baba alikuwa ni mngoni lakini mama yangu alikuwa ni msambaa pyuwa. Kilichotupeleka Tanga ni kuzuru na kustarehe, yaani 'bata batani' vijana wa kisasa husema. Tulizunguka, tulitembea, tulikula na kunywa vyakula vya asili ya Tanga. Tulienda kuzuru Mapango ya Amboni. Huko tuliipata elimu ambayo pengine hakuna mahali tungeipata. Wacha nikupitishe kidogo mapangoni.

AMBONI-TANGA.

Tulifika kwa usafiri wetu, hapo tulielekezwa na mlinzi mwenye tabasamu mwanana mahali pa kuegesha gari. Tulishuka kwenye gari na kujinyoosha miili. Macho yetu yalikutana na mandhari nzuri sana. Mianzi iliyo na afya iliyoota kando ya kijito kilichokuwa pembeni mwa njia, ilifanya mahali pale pawe na rangi nzuri na mvuto wa kipekee sana. Tulijiandikisha kwenye daftari la kumbukumbu na hapo tukapewa mtaalamu wa kutuongoza mapangoni. Alibeba kabegi kenye vifaa fulani na kamera mkononi. Tulitoka kwenye nyumba ya utawala na kuelekea tulikoelekezwa. Lango la pango lenye muundo wa ramani ya Afrika kilikua kituo namba moja cha kuchukulia picha. Muongozaji alibobea kwenye swala zima la uchukuaji wa kumbukumbu kwa namna iliyotufurahisha wote. Alitupiga picha kwa awamu kisha alitupiga ya pamoja. Alitufundisha 'mapozi' yaliyofanya tuanze kuifurahia safari mapema sana. Tuliingia ndani na kukutana na chemichemi itiririkayo maji majira yote ya mwaka. Mwamba wake ulimeremeta na maji yaliyotiririka pale yaling'ara sana. Maajabu ya mwamba huo ni kwamba unaongezeka ukubwa kila baada ya muda fulani. Maswali tuliuliza na jibu la muongozaji liliturudhisha. "Mwamba huu unakuzwa na mabadiliko ya kikemikali kutoka kwenye miamba ya chokaa, huongezeka kiasi cha milimita saba kwa miaka mia moja" tulistaajabu na kufurahia miujiza ya Mungu.

Tulichukua picha za kumbukumbu. Tulipita kwenye kilinge ambacho wajuzi wa hizo kazi hukitumia kufanyia ibada za miungu ya asili. Baada ya hapo tulipatiwa kila mmoja kurunzi lake; tukapita kwenye njia nyembamba, wenyewe huifananisha na njia ya mbinguni japo hakuna mwenye uhakika. Tuliendelea kuperuzi miujiza ya Mungu, tulifika mahala kuna michoro mbalimbali ambayo hakuna binadamu aliyehusika kuichora. Imetengenezwa kwa alama zilizoachwa na popo walioanza kuishi humo zamani sana. Kiukweli, hapa tulitazamana kimbea sana na Sunche kisha nikamchekea mdogoangu ambaye naye hakuamini maelezo ya jamaa aliyetuongoza kuyatalii mapango yale. Kulikuwa na mchoro wa mnyama chui ulioonekana juu kabisa umbali wa mita ishirini na sita kutoka tulipokuwa tumesimama. Sambamba na hiyo, kulikuwa na picha ya unyayo mkubwa wa mguu ufananao na wa binadamu. Kiukweli palivutia mno macho yetu.

Maajabu hayakuishia hapo, tulikutana na miamba yenye maumbo yafananayo na maungo ya mwanamke; matiti na nanilii. Tuliona mwamba wenye umbo la mbawa ya tai, nzuri zaidi tukamuona mamba akiogelea mapangoni! Bila shaka hata wewe umeshtuka, tulishtushwa pia na picha kubwa ya mnyama mamba aliyeonekana akiogelea. Miamba ilionekana ya miujiza mingi sana. Tuliona mchoro wa bao la kete ulioonekana umbali wa futi kumi na tano juu ya pango. Tulizidi kustaajabu. Tulipita njia moja mbaya mno, huo ubaya wake pia ni kivutio, tulilazimika kusaidiana kupanda, paliteleza ila palipitika. Tulifika mahali pa giza totoro. Tulilionja giza baada ya kiongozi wa msafara kututaka tuzime kurunzi. Nilimkamata vilivyo Sunche na sikuacha kuongea ili kuhakikisha sitorokwi pale. Niliipata hisia ya upofu kwa mara ya kwanza maishani. Nilimshukuru Mungu kwa kunipa uoni.

Tuliwasha kurunzi na hapo maelezo kuhusu eneo lile yakatolewa. Kushoto kwake ni njia ya giza ambayo kwa karne hii hakuna aliyefanya jaribio la kuipita baada ya tetesi za mtalii wa Kizungu kupotelea huko akiwa na mbwa wake ambaye alipatikana miezi mingi baada ya kupotea huko nchini Kenya. Hadithi ya kutoweka kwa mzungu yule haijapata mwendelezo, hakupatikana yeye wala masalia ya mwili wake. Tuliogopa na kuchagua kuelekea kulia.

BURUDIKA
www.kitabumarket.co.tz

# KALAMU YANGU
## Kitabu: Dira Ya Moyo—Laura Pettie

Karibu katika safu yetu mpya ya KALAMU YANGU, ambapo waandishi mbalimbali watatueleza juu ya vitabu vyao walivyoviandika. Katika safu hii Ngurumo ya Mwandishi linachokonoa kujua 'kwanini' aliandika hivi, kilichomsibu nini na mengine mengi.

Katika Toleo hili la XLIX (49) tunaanza na mwanadada Laura Pettie, Mshindi wa Tuzo ya Nyerere ya uandishi bunifu msimu wa pili. Haya ni mahojiano aliyoyafanya na mwandishi wetu...



**Ngurumo:** Tueleze mantiki ya kuandika kitabu Dira ya Moyo, yaani kitu kitu Gani kilikusukuma?

**Laura:** Kuna mambo kadhaa yalinisukuma kuandika riwaya ya Dira ya Moyo. Kwanza kabisa ilikuwa ni kutaka kuishuhudia ile tofauti iliyopo kati ya mitazamo ya kijamii, yaani vile vitu ambavyo tunaviamini na uhalisia wa maisha ulivyo. Niliangalia watu wengi wanaamini nini linapokuja suala la ndoa na vipengele vyake kama vile kupendana, kuvumiliana, kuhitajiana na hata kuachana. Kuna namna niliona katika uhalisia wa maisha kuna sehemu hatuyaishi yale tunayoyaamini.
Kabla ya kuandika, nilipata kuwauliza maswali watu kadhaa, wenye ndoa na wasio na ndoa, kuhusu kuvunjika kwa ndoa ya miaka 25. Sikupata jibu lililosapoti ndoa ya aina hiyo kuvunjika. Nilipata majibu yaliyonionyesha kuwa ndoa ya aina hiyo haina sababu ya kuvunjika kama hakuna hali ya unyanyasaji, ambao wengi waliutafsiri kama kipigo.
Baada ya hayo majibu, nilirudi mezani nikasema sasa nitaandika mkasa, kisha nione kama msimamo utabaki kuwa uleule ama utayumba. Ninakuhakikishia, asilimia kubwa ya wasomaji waliopata bahati ya kuisoma riwaya hii pasipo kujali *marital status* zao, wakiwemo wale niliowauliza maswali kuhusu kuvunjika kwa ndoa ya miaka 25, walisapoti ndoa ya Rex na Ramla kuvunjika. Ndoa ya miaka 25 ambayo haikuwahi kuwa na unyanyasaji wa aina yoyote ile. Je, nini kiliwabadili mawazo? Ni mkasa uliopo ndani ya Dira ya Moyo? Au ni kweli wanachoamini ni tofauti na kile wanachokiishi au kukitamani?

Mbali na hilo, nilitaka kugusia mambo kama tofauti kubwa ya umri baina wa wapendano wawili, changamoto za kuingia katikati ya mapenzi yaliyosimama na kuhalalishwa, suala la kutoka kwenye familia yenye imani kali linavyoweza kumfunga mtu kuuishi uhalisia wake na mengine mengi.

**Ngurumo:** Je uliyoyaandika yana uhusiano wa moja kwa moja na maisha ya watu fulani?

**Laura:** Naweza kusema ndiyo, na pia naweza kusema hapana. Nikisema ndiyo, namaanisha kuwa ndani ya Dira ya Moyo nimeyamulika maisha ya Rex Makaula kama mtu maarufu, ambapo maamuzi kwenye maisha yake binafsi nje ya kazi iliyompa umaarufu, hayaishii ndani mwake tu. Vyombo vya habari vinamwandama, na athari ya yeye kuwa maarufu inawaumiza mpaka wale wasiohusika. Hali kadhalika, familia ya Mchungaji Kante inawakilisha watu wa kiroho. Kama unavyojua, wao hutazamwa kama nusu ya malaika. Sasa mtoto wa nusu ya malaika anapoingia kwenye skendo ya uzinzi, hili si anguko la mtoto pekee inaweza kuathiri mpaka namna watu watakavyomchukulia mtumishi huyo. Yote kwa yote, nimejaribu kuonyesha nje ya vyeo na umaarufu, wahusika bado ni binadamu kama watu wengine.
Nikisema hapana, ninamaanisha hii ni simulizi ya kutunga, haina uhusiano wowote na tukio lolote la kweli. Ijapokuwa wengi wanaoisoma wanaona kama kuna namna inawezakana mhusika mkuu akawa mwandishi mwenyewe. *Hahahaaa!* Kwa sababu mhusika kama Samwel Kwame nimewahi kumtambulisha mahali kuwa ndiye huyu mliyemsoma katika Dira ya Moyo. Ni kweli

anaitwa jina hilo, na ni kweli ni raia wa Ghana. Kwa hiyo, kujitetea kwamba ni utunzi kwa asilimia 100 inakuwa ngumu tena. Lakini, ninakuhakikishia hii ni kazi ya utunzi tu.

**Ngurumo:** Tueleze Sasa mtiririko wa matukio halisi nje ya kitabu uliyokutana nayo wakati unaandaa kazi hii mpaka inatoka kitabuni - Panda shuka za hapa na pale, makwazo, kutiwa moyo, kukata tamaa na mpaka mafanikio -

**Laura:** Kama nilivyokwambia awali, nilianza na utafiti kwanza, kisha ndipo nikaandika. Haikuwa kazi ngumu sana kuiandika stori kwa sababu haikuwa riwaya ya kwanza kuandikwa nami.

Changamoto kubwa ilikuwa ni ile kujua kwamba hiki kinaenda kuwa kitabu. Kwa asilimia zote kitasomwa na wazazi hususani mama yangu. Sasa kuandika sehemu za mahaba na mapenzi kuna wakati nilitamani kuondoa vipande hivyo. Machoni pa mzazi, kila mtoto ni mtakatifu. Au siyo? Sasa kuuvunja huo utakatifu nilihitaji kufanya maamuzi magumu, nayo ni kuwatazama wazazi wangu kama wasomaji tu. Haikuwa kazi rahisi, lakini hatimaye niliweza. Nikaandika pasipo hofu yoyote.

Pia, nimetumia mchangayiko wa nafsi kwenye kusimulia. Nimetumia nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Kwa kiasi fulani ulihitajika umakini mkubwa ili nisichanganye. Hii ilikuwa sehemu ya changamoto kubwa wakati wa kuhakikisha nimeandika kazi inayoeleweka.

Changamoto ya mwisho, ilikuwa ni namna kuimaliza riwaya. Mwanzo nilidhani kazi hii ingekuwa rahisi tu, kwa kuwa siku zote mimi ni *Pantser,* yaani mwandishi ambaye anaandika kulingana na kile kinachomjia kichwani, huwa sipangi mapema kazi iweje. Lakini, kwenye kuandika mwisho wa Dira ya moyo ilibidi niwe *Plantser*, yaani nipange mwisho uweje. Hii ilifanya nitumie muda zaidi kupitisha aina tatu za mwisho nilizopanga, kwa kuangalia kwanza faida na hasara zake. Hakika sijawahi kujutia mwisho niliouchagua.

Sasa namna kitabu hiki kilivyohaririwa mpaka kuingia sokoni ni stori ya kipekee inayojitegemea, lakini kwa dhati kabisa niwashukuru Fadhy Mtanga na Maundu Mwingizi kwa mwongozo na usimamizi ambao, nakiri ulifanya nisipitie changamoto kubwa kwenye uchapishaji na usambazaji.

Kuhusu mafanikio, najivunia kukiona kitabu hiki katika maktaba za vyuo vikuu vikubwa mbalimbali kama Chuo kikuu cha Indiana nchini Marekani, na pia kutumika kwake kwenye utafiti wa fasihi ya lugha ya Kiswahili katika chuo kikuu cha Warsaw, nchini Polandi.

Kwa kweli, ilinipa moyo wa kujiimarisha zaidi kwa kazi iliyofuata. Hivyo, si tu kwamba ni kazi ya kwanza kunitambulisha sokoni, ingawa si ya kwanza kuandikwa, bali pia Dira ya Moyo ilifungua njia nzuri kwa vitabu vyangu vilivyofuatia.

Ngurumo: Laura Pettie ni mwandishi wa kike wa kizazi hiki. Kalamu yake iliyotoa mafunzo mengi kwenye kitabu cha Dira ya Moyo ndiyo iliyotoa burudani isiyopimika katika kitabu cha Kiroba Cheusi. Lakini ndiyo iliyompa ushindi mkubwa katika Tuzo ya Nyerere ya Uandishi Bunifu msimu wa pili.

Ukipata bahati ya kukutana naye, kamwe huwezi kumdhania kama ndiye aliyejawa maneno mengi viganjani mwake. Laura ni mpole, mkimya, ataayekupa majibu ya maswali yako kwa kukutazama tu. Lakini pia ni kiumbe hadimu kuonekana hadharani hasa kwenye matukio yasiyo na tija kwake.

Ukitaka kumjua vyema usisite kumtembelea katika kurasa yake ndani ya faebook kwani hapo hujimwaga akamwagika.

Ni mmoja kati ya waandishi wanaotoa mafunzo ya maisha kila siku kupitia kurasa wake wa facebook na pia yu mstari wa mbele katika kuisaidia jamii kwa kufanya harambee mbalimbali kupitia rafiki zake.

Toleo lijalo, tutakusogezea kazi nyingine ya 'mwanamama' huyu. Usitoke hapa, endelea kubaki!



## Tangazo

**Lini ?**




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com